SportPesa
TZS. 450,150,500
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Hoja** 11 zenye kero katika Muungano zaondolewa rasmi

UKURASA 5




UKURASA 11

Jumatano Agosti 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580683

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

# Askofu: Kila padri apate chanjo corona

•**Awataka** waumini wawapuuze wanaowapotosha... *Endelea ukurasa 2*



Askofu Mkuu Mwandamizi, Jude Thadeus Ruwa'ichi.



UKURASA 2

Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Jerry Silaa

## Silaa atinga na sanduku, Biblia kuhojiwa na Kamati ya Bunge

UKURASA WA 3

### KESI NYINGINE TOZO MIAMALA YAPINGWA

SERIKALI imeiomba Mahakama kutupilia mbali shauri la kupinga tozo ya miamala ya simu lililofunguliwa na Charles Odero, kwa madai kanuni ziko kwa mujibu wa sheria na malalamiko yake...



UKURASA WA 3

### TAREHE YA HUKUMU YA SABAYA YATANGAZWA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imetangaza kuwa Oktoba Mosi, mwaka huu itatoa hukumu katika kesi ya jinai namba 105 inayomkabili...

UKURASA WA 4

### DED, MAOFISA UGAVI WAHOJIWA TUHUMA WIZI

WATU wanane akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Asajile Mwambambale, wanahojiwa na Jeshi la Polisi...



UKURASA 3

Majeneza yenye miili ya maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa mikoa ya Mbeya na Songwe, yakiwa yamepangwa kwenye viwanja vya mamlaka hiyo, jijini Mbeya jana, kwa ajili ya kuagwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## VILIO VYATAWALA MIILI MAOFISA TRA IKIAGWA

**MICHEZO** HITIMANA, OMOG WATAJWA KUMRITHI BADRU MTIBWA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mahakama Kuu yamaliza mgogoro wa Kanisa Sloam

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imemaliza mgogoro wa muda mrefu wa Kanisa la Sloam dhidi ya Elisha Eliya, aliyekuwa akidaiwa kupora mamlaka ya kanisa hilo bila utaratibu.

Hukumu ilisomwa mbele ya Jaji Leila Mgonya, mahakama imetoa zuio la kudumu dhidi ya Eliya na mawakala wake, kutotakiwa kujihusisha na utawala wa kanisa hilo lijulikanalo kama Huduma ya Kimataifa ya Sloam.

Mgogoro huo unadaiwa kuanza baada ya kifo cha mwanzilishi, Mtume na Nabii Nduminfoo Zebedayo Munuo, kwa jina maarufu Eliya na Adam wa Pili au Mungu wa Majeshi aliyetwaliwa na Mungu Novemba 16, 2014, Elisha Eliya ambaye alijipa madaraka ya kumrithi kiongozi huyo bila kufuata utaratibu wa Katiba yake.

Kutokana na hatua hiyo, Elisha Eliya maarufu kama Miaka 1000, kulisababisha mgawanyiko wa waumini na aliwashawishi baadhi waliomuunga mkono na wakapora mali mbalimbali za huduma yakiwamo majengo ya ibada.

Pia Miaka 1000 alijaribu kubadili usajili wa huduma hiyo kwa jina la The Pool of Sloam Church, lakini akakwama hivyo Bodi ya Wadhamini ililazimika kumshtaki Mahakama Kuu ya Tanzania, kupitia kesi ya madai namba 24 ya mwaka 2007.

Katika hukumu iliyosomwa baada ya kusikiliza shauri hilo upande mmoja, mdaiwa Eliya hakufika mahakamani, mahakama ilikubaliana na maelezo ya wadai na ikatoa amri walizokuwa wakiziomba.

"Mahakama hii inatoa amri ya zuio la kudumu dhidi ya Elisha Eliya, mawakala wake, watumishi wake na mtu yeyote atumikae kwa niaba yake kutokutumia na kutokusajili jina la The Pool of Sloam Church au Kanisa la Sloam mahali popote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Mahakama inaamuru Eliya maarufu Miaka 1000 kwa kuwa hakuwa kiongozi wa kikatiba haruhusiwi kufanya shughuli za kiutawala zikiwamo kuwateua au kuajiri makuhani au waumini.

"Elisha Eliya Miaka 1000 au yeyote anayetumika kwa niaba yake kukabidhi mara moja, maeneo, viwanja, majengo na mali zote za SMI walizokuwa wanazitumia kwa jina la SMI au The Pool of Sloam Church na kulipa gharama zote za kesi hiyo," alisema Jaji Leila.

Katika kesi hiyo Bodi ya Sloam iliwakilishwa na mawakili tofauti katika hatua mbalimbali akiwamo Jerome Msemwa aliyehusika katika hatua ya mwisho ya usikilizwaji wa ushahidi.

Awali Miaka 1000 kupitia kwa wakili wake Sweetber Nkuba, aliwasilisha maelezo yake ya utetezi wa maandishi.

Katika maelezo hayo alikana madai yote akidai kuwa hakukaa kutii maelekezo ya serikali na kwamba wala hapakuwapo na ukiukwaji wa Katiba ya Sloam kama ilivyoelezwa na mdai.

Zaidi alidai kuwa hapakuwapo na aina yoyote ya udhalilishaji kutokuwa na imani dhidi ya mdaiwa na kwamba mdai anapaswa kuthibitisha madai yake hayo.

Maelezo hayo ya maandishi ya mdaiwa yalitupiliwa mbali na Mahakama Machi 27, 2020 baada ya mdaiwa kutokufika mahakamani wakati wa usuluhishi, hivyo mahakama ikaamuru kesi kuendelea na usikilizwaji wa upande mmoja.

# Askofu Mkuu amtaka kila padri apate chanjo corona

**Na Romana Mallya**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu la Kanisa Katoliki Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi, amewaagiza mapadri wote kwenda kuchanjwa chanjo ya corona na kuachana na wanaopiga kelele za kuipinga.

Kiongozi huyo wa kiroho aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa adhimisho la misa takatifu kumwombea Padri Paul Haule iliyofanyika Kanisa la Mt. Petro Oysterbay, Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Padri Haule alikuwa Paroko Msaidizi wa Parokia hiyo ya Mt. Petro na Mkurugenzi wa Tumaini Media ambaye alifariki dunia Jumatano iliyopita, Hospitali ya Kardinali Rugambwa, Ukonga.

Katika misa hiyo, Askofu Ruwa'ichi alisema kuwa kipindi wanachopita sasa ni kigumu, tete na kinachohitaji uwajibikaji wa hali ya juu.

"Kwa sababu hiyo ninaomba niwahimize katika haya yafuatayo... Kwanza; zingatieni sana maelekezo ya wataalamu wa afya, nisianze kuyataja hapa moja kwa moja.

"Lakini, nimwombe kila mmoja wenu ajitume na awajibike sana katika kuyaishi na kuyafanyia kazi maelekezo ya wataalamu wa afya," alisema.

Askofu huyo alisema jambo la pili anawaalika ambao wana umri unaostahili kuchanjwa, waende wakachanjwe, akisisitiza kuwa hiki ni kipindi ambacho kuna maneno mengi kuhusu chanjo ya corona.

"Ninaomba niwaambie kwamba kati ya waliotutangulia kuchanjwa ni Baba Mtakatifu Francis, ametupa mfano wa kuchanjwa yeye mwenyewe.

"Mimi nimewapa mfano wa kutangulia kwenda kuchanjwa, nilikuwa miongoni mwa Watanzania wa kwanza kuchanjwa.

"Ninaomba nirudie kusema, mwaka jana tulimwomba Mungu atujaalie kupatikana kwa chanjo dhidi ya COVID-19 (corona), sasa chanjo imepatikana na tumeingia kwenye malumbano ya kuanza kusema haya na yale dhidi ya chanjo," alionya.

Aliwataka wasingojee mpaka mambo yawatinge watumie vizuri fursa ambazo Mungu aliwapa kwa kuhakikisha wanajitunza na kujihami.

"Kwa sababu hiyo, sijui ni mapadre wangapi mmshechanjwa. Lakini leo (jana) ninaomba nitoe agizo, kila padre akachangwe, kila padre akachanjwe, tusifanye utoto, tusifanye lele mama, hii COVID haina mjomba na shemeji, inatuumiza.

"Inatuondolea uhai, ninaomba niwakumbushe ni utashi wa Mungu kwamba tuwe hai na tuwe na uhai tele. Kwa hiyo tuujali huo uhai. Wale wanaopiga ndaro (maneno ya kujisifu), kina Gwajima, achacheni nao.

"Achaneni nao kabisa, hayo mazungumzo ya wanayotia shaka, wanaopinga, hayo ndugu zangu muyaweke pembeni, sasa tujihami na tuendelee kumwomba Mungu atuhurumie, atunusuru, atuondolee hili janga," alihitimisha.

Hivi karibuni kumeibuka mvutano kati ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima na Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, baada ya kiongozi huyo kushauri wananchi wasipewe chanjo ya corona kwa kuwa anaamini ina madhara kiafya.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na kumpongeza Rais Mpya wa Zambia, Hakainde Hichilema, baada ya kuapishwa kuwa Rais wa saba wa Zambia, katika Uwanja wa Taifa wa Mashujaa, jijini Lusaka, Zambia jana. **PICHA: IKULU**

# Silaa atinga na vitabu, biblia bungeni kuhojiwa

**Na Augusta Njoji,**

DODOMA

MBUNGE wa Ukonga, Jerry Silaa (CCM), amehojiwa na Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, akifika mbele ya kamati hiyo akiwa na vitabu 11 vikiwamo vya masuala ya kodi na biblia.

Silaa aliingia kwenye ukumbi wa mahojiano jana saa 8:43 mchana, kamati hiyo ikiwa chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Emmanuel Mwakasaka.

Baada ya kukaribishwa kwenye ukumbi wa kamati hiyo, Silaa aliingia na kuweka begi lililokuwa na vitabu na kuketi kwenye kiti kilichoandaliwa kisha kupuliza kitakasa mikono kwenye kipaza sauti.

Hata hivyo, kutokana na wingi wa vitabu alivyoingia navyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwakasaka, alimwomba kuvisogeza pembeni kidogo ili aonekane vizuri kwa wajumbe.

Mbunge huyo alifika kwenye geti la Bunge saa 6:49 mchana akiwa kwenye gari jeusi aina ya Lumio huku akiwa amebeba begi jeusi, chupa ya maji na vitabu vitatu mkononi ikiwamo biblia.

Akiwa katika geti kubwa la kuingia, Silaa aligoma kusindikizwa na askari kama ilivyokuwa juzi kwa Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, na kutaka aonyeshwe kanuni inayotaka yeye asindikizwe na askari kwenye kamati hiyo.

Ofisa Mwandamizi wa Usalama Bungeni, Peter Magati, alimweleza mbunge huyo kuwa Bunge linaendeshwa kwa utaratibu, kanuni, sheria na miongozo.

Hata hivyo, baada ya maelezo hayo, Silaa alikubali kuongozana na askari hao ambao walikuwa wawili, mmoja akiwa amevaa kiraia na mwingine sare za Jeshi la Polisi na kuonyeshwa eneo la kupumzikia lililoko jengo la utawala kabla ya kuitwa kwenye kamati.

Mbunge huyo alikaa kwenye eneo hilo la mapumziko kwa takriban saa mbili akisubiria kuitwa.

Silaa alihojiwa kwa zaidi ya saa mbili na atarejea tena kesho kumalizia mahojiano na kamati hiyo.

Mwakasaka alisema Silaa alihojiwa kwa mambo machache na atahojiwa tena kesho.

Akizungumza baada ya kuhojiwa na kamati hiyo, Silaa alisema wabunge wakati wote wanapotekeleza majukumu yao, hasa wa CCM, wana wajibu wa kumsaidia Rais.

HABARI KITAIFA

# Vilio vyatawala miili maofisa TRA ikiagwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MIILI ya maofisa watano wa Mamlaka ya Mapato (TRA) mikoa ya Mbeya na Songwe waliofariki dunia kutokana na ajali ya gari, imeagwa jijini Mbeya huku vilio na simanzi vikitawala miongoni mwa ndugu na jamaa wakiwamo maofisa wa serikali.

Maofisa hao ni: Benard Mshingi (40), Ofisa wa Forodha Mkoa wa Songwe; Azaria Sivonike (42), Dereva wa TRA Mkoa wa Mbeya; Joel Mitondwa (36); Said Buddy (34); na Fahadi Haji (26) ambao wote ni maofisa wa Forodha Mkoa wa Mbeya.

Miili hiyo iliagwa jana kwenye viwanja vya Ofisi ya TRA Mkoa wa Mbeya baada ya kusafirishwa kutoka katika Hospitali ya Mkoa wa Songwe iliyoko Vwawa.

Miili hiyo iliwasili katika eneo hilo na kisha kupangwa katika eneo moja lililokuwa limeandaliwa kwa ajili ya kuagia ambapo baada ya miili hiyo kuwasili, waombolezaji waliokuwa wamejazana kwenye eneo hilo walianza kuangua vilio.

Wakati wa kuaga miili hiyo, baadhi ya ndugu wa marehemu hao walianguka na kupoteza fahamu, hivyo kuwapa ugumu wa kazi maofisa wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kitengo cha Miradi waliokuwa wanalinda eneo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ambaye aliongoza waombolezaji kuaga miili hiyo, aliwafananisha vijana hao na makamanda wa jeshi kwa maelezo kuwa walifariki dunia wakati wakilipambania taifa lao.

Alisema walikuwa wanapambana kukusanya kodi kwa ajili ya kuiwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Homera aliwataka maofisa wengine wa serikali kufanya kazi kwa kujituma ili kuhakikisha wanawatumikia wananchi kwa mujibu wa miongozo.

"Walikuwa wanapambana ili watoto wetu wasome elimu bure, walikuwa wanapambana ili tujenge vituo vya afya, walikuwa wanapambana ili tujenge barabara, hivyo ninaomba tuendelee kuwaombea kwa Mungu ili wapumzike mahala wanapostahili," alisema Homera.

Aliwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa maofisa hao huku akiwataka wawe wavumilivu katika kipindi hiki cha majonzi na kuwataka waombolezaji kuwaombea marehemu.

Awali akisoma wasifu wa marehemu hao, Mkurugenzi wa Utawala wa TRA, Michael John, alisema vijana hao kwa asilimia kubwa walikuwa na umri mdogo na waliaminiwa na mamlaka hiyo kutokana na uchapakazi wao.

Mkurugenzi huyo alisema mkubwa kuliko wote alikuwa na umri wa miaka 42 lakini wengine wote walikuwa na miaka kuanzia 40 kushuka chini na kwamba walikuwa wanasaidia kupambana na magendo katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Mbeya na Songwe.

"Kwa niaba ya Kamishna wa TRA, ninaomba niwaambie kwamba tumepoteza nguvu kazi kubwa mno, tunawapa pole sana ndugu, jamaa na marafiki wa ndugu zetu hawa," alisema Michael.

Baada ya kuagwa, miili ya maofisa wawili ambao ni Haji na Buddy ilisafirishwa kwa ndege kwenda Dar es Salaam ambapo Haji anatarajiwa kuzikwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi visiwani Zanzibar na Buddy anatarajiwa kuzikwa Chalinze mkoani Pwani.

Miili mingine miwili inatarajiwa kusafirishwa kwa ndege kwenda Dar es Salaam na mmoja utasafirishwa kwenda kuzikwa katika Wilaya ya Makete mkoani Njombe.

Maofisa hao walifariki dunia juzi alfajiri katika eneo la Hanseketwa wilayani Mbozi mkoani Songwe baada ya gari walilokuwa wanalitumia kugonga lori kwa nyuma ambapo wanadaiwa kuwa walikuwa wanalifukuza gari lililodhaniwa kubeba bidhaa za magendo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akiongoza waombolezaji kuaga miili ya maofisa watano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), jijiji Mbeya jana, waliofariki kwa ajali mkoani Songwe. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Hukumu ya Sabaya Oktoba Mosi

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imetangaza kuwa Oktoba Mosi mwaka huu itatoa hukumu katika kesi ya jinai namba 105 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34) na wenzake wawili.

Kesi hiyo ya jinai ilinguruma kwa siku 37 hadi jana baada ya shahidi wa tatu wa utetezi kukamilisha kutoa ushahidi wake katika mahakama hiyo.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wote wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Hakimu Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, alisema jana kuwa Oktoba Mosi mwaka huu mahakama hiyo itatoa hukumu ya kesi hiyo baada ya kusikiliza mashahidi wa pande zote mbili na kupokea vielelezo vya ushahidi.

Baada ya mahakama hiyo kufunga ushahidi wa utetezi, Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, alidai kwamba kesi hiyo imefikia tamati, hivyo wanaomba mahakama ifanye majumuisho kwa njia ya maandishi kulingana na ushahidi uliotolewa na mashahidi. Vilevile, Wakili Kweka aliiomba mahakama kupewa siku saba hadi Septemba Mosi mwaka huu kwa ajili ya kufanya majumuisho hayo na kuyawasilisha mahakamani.

Kutokana na maombi hayo, hakimu aliagiza majumuisho kwa njia ya maandishi yafikishwe mahakamani huko ndani ya wiki moja kuanzia jana na kubainisha kuwa hukumu ya kesi itatolewa Oktoba Mosi mwaka huu.

Wakili wa Utetezi, Dancan Oola, alidai mahakamani huko kwamba watawasilisha majumuisho yao kwa njia ya maandishi na tayari kwa ajili ya kupokea tarehe ya siku ya kutolewa kwa hukumu ya kesi hiyo.

Inadaiwa kwamba Februari 9, mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, washtakiwa hao waliiba fedha Sh. milioni 2.769, mali ya Mohamed Saad na baada ya wizi huo walitumia silaha ya bunduki kuwatisha waliokuwa kwenye duka hilo.

Katika shtaka la pili, inadaiwa washtakiwa hao kwa pamoja, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. 390,000, mali ya Bakari Msangi, na baada ya wizi huo walimfunga na pingu, wakampiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia silaha ya bunduki kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake.

Inadaiwa katika shtaka la tatu kwamba Ole Sabaya na wenzake hao, Februari 9 mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja aina Tekno Pop 1 na fedha kiasi cha Sh. 35,000, mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wapatiwe fedha na mali walizoiba.

# Kesi nyingine tozo miamala yapingwa

**Na Kulwa Mzee**

SERIKALI imeiomba Mahakama kutupilia mbali shauri la kupinga tozo ya miamala ya simu lililofunguliwa na Charles Odero, kwa madai kanuni ziko kwa mujibu wa sheria na malalamiko yake yanapaswa kusikilizwa na Mahakama Kuu ikikaa kama Mahakama ya Kikatiba na si Mahakama Kuu ya kawaida.

Wakili wa Serikali Mkuu, Gabriel Malata, ndiye aliyewasilisha pingamizi hilo jana mbele ya Jaji John Mgeta.

Odero alifungua kesi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Fedha na

Mipango akipinga kanuni za tozo kwa madai hazikufuata utaratibu wa kufunguliwa, inavunja misingi ya Kikatiba inayohusisha ushirikishwaji wa wananchi kutoa maoni kwamba tozo ni kubwa.

Wakili Malata alidai kanuni zipo kwa mujibu wa sheria, uamuzi umelenga kuiwezesha serikali kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati.

Alidai kanuni zilikuwa shirikishi kwani zilishirikisha wawakilishi wa wananchi.

Upande wa Serikali uliendelea kudai kanuni husika zina mamlaka kisheria na kikatiba katika uanzishwaji, na pia madai hayako sawa mbele ya Mahakama, kwani yana mapungufu mengi kisheria ikiwamo mlalamikaji kushindwa kuonyesha kwa namna gani ameathiriwa na kanuni.

Serikali inadai malalamiko yaliyopo mahakamani yanahusu uvunjwaji wa Katiba na sheria ambayo yanaweza kusikilizwa na Mahakama Kuu ikikaa kama Mahakama ya Kikatiba na si Mahakama Kuu ya kawaida.

Pia ilidai ushahidi wa kiapo una upungufu, kwani umejikita katika maneno ya kusikia, maoni binafsi, mambo ya kisheria ambayo hayakubaliki kwenye ushahidi wa shauri kama hilo.

Akijibu hoja hizo Wakili wa Odero, John Seka, alipinga hoja za serikali akidai kwamba hazina msingi wowote, na kwamba madai yao yana msingi kuwepo mahakamani.

"Tunasubiri Mahakama itupe uamuzi sahihi, ikiwa itakubaliana na hoja zetu tutaomba kesi ya msingi ya kupinga tozo isikilizwe," alisema.

## Madarasa mapya 428 kujengwa Desemba

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI ya mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu, imeanza kuweka mikakati ya kujenga vyumba vya madarasa 506, ili kuondokana na upungufu uliopo kwa ajili ya wanafunzi 25,300 watakaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Katibu Tawala Msaidizi, Mipango na Uratibu wa Mkoa wa Morogoro, Anza Amen Ndossa, alisema hayo mjini hapa jana kwenye kikao cha kujadili mkakati wa kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022 kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa, Martine Shigella.

Ndossa alisema kutokana na upungufu wa madarasa hayo, mkoa unalazimika kuanza mapema kuunganisha nguvu za viongozi kuhamasisha wananchi na wadau wa elimu kujenga kwanza vyumba 428 vya madarasa ya shule za sekondari kabla ya mwezi Desemba, mwaka huu.

"Ni lazima tuanze kujipanga hivi sasa katika ujenzi huo kwani baadhi ya wanafunzi watashindwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa kukosa vyumba vya madarasa," alisema Ndossa.

Alisema uchambuzi wa bajeti za halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/22 unaonyesha kuwa halmashauri kwa upande wa shule za sekondari zimetenga fedha za ujenzi wa vyumba 34, ukamilishaji wa vyumba 44 vya madarasa, hivyo kufanya upatikanaji wa vyumba vipya 78. Pia alisema kwa hali hiyo, kutokana na matokeo ya wanafunzi mkoa utakuwa na upungufu wa vyumba 428.

Kutokana na taarifa hiyo, Shigella aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na wenyeviti wa halmashauri kuweka mikakati ya namna watakavyokabiliana na upungufu wa vyumba hivyo kwa kuzingatia rasilimali za kila halmashauri kabla au ifikapo Desemba, mwaka huu. Aliwaagiza kuwa na utaratibu wa ujenzi wa madarasa kuanzia Julai ili kuondoa tatizo la wanafunzi kukosa sehemu ya kwenda kutokana na ukosefu wa madarasa.

"Kwa nini tusijipange kuanzia Julai tukaanza kujenga kidogo kidogo kwa nguvu za wananchi na halmashauri yenyewe? Sasa hivi tupo mwezi wa nane tunaingia wa tisa. Tuna miezi mitatu ya kujipanga vizuri ili matokeo yakitoka jambo hili liwe limekamilika," alisema.

# DED, maofisa ugavi wahojiwa tuhuma wizi mabati ya shule

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WATU wanane akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Asajile Mwambambale, wanahojiwa na Jeshi la Polisi mkoani Morogoro wakituhumiwa kuhusika na wizi wa mabati 1,172 katika mazingira ya kutatanisha.

Mabati hayo yalikuwa yamehifadhiwa kwenye stoo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwa ajili ya kuezeka Shule ya Msingi Kidete. Watu wengine wanaohojiwa na polisi ni maofisa ugavi wanne na madereva watatu wa halmashauri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fortunatus Musilim, amekiri kukamatwa na kuhojiwa kwa watuhumiwa hao na kwamba tukio hilo lilitokea Juni 17, mwaka huu, kwenye stoo ya halmashauri ya wilaya maeneo ya Ujenzi, kijiji cha Mbumi B wakati mabati hayo yalipochukuliwa ili kupelekwa shuleni Kidete kwa ajili ya kuezeka vyumba vya madarasa.

Asajile, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, kwa mujibu wa Musilimu, anatuhumiwa kuhusika na wizi huo wa mabati wakati akiwa mkurugenzi wa halmashauri hiyo.

Musilimu alisema fedha kwa ajili ya ununuzi wa mabati hayo yenye thamani ya Sh. 31,408,500 zilitolewa na halmashauri kwenda katika shule husika, lakini baadaye yalirudishwa kijanja katika halmashauri na baadaye kutoweka bila stoo kuvunjwa.

"Mabati yaliibwa kwenye stoo ya halmashauri lakini milango haikuvunjwa wala makufuli hayakuvunjwa. Hakukuwa na uvunjaji wowote lakini mabati yalitoweka," alisema.

Kamanda Musilimu aliwaonya watumishi wote wa umma kujiepusha na vitendo vya wizi na ubadhirifu wa mali za umma na kwamba yeyote atakayebainika kufanya vitendo hivyo na akabainika, atachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Waziri Mkuu ameshatoa maagizo kwenye kikao chake kwa njia ya video kwa wakuu wa mikoa kuhusu kuhakikisha kunakuwapo usimamizi mzuri wa mali za serikali na miradi ya kimkakati, miradi ya elimu, barabara na afya.

Mimi kama mjumbe wa kamati ya ulinzi na usalama nimesikia maelekezo hayo, hivyo nawaonya yeyote atakayebainika kuhusika na wizi na ubadhirifu kwa mkoa wa Morogoro hatakuwa salama. Ulinzi wa Morogoro ni wetu sote, wahalifu wote tutawasaka katika kila eneo," alisema.

Taarifa zaidi kutoka Kilosa zimetaja waliohojiwa mbali na Mwambambale, ni Mkuu wa Kitengo cha Ugavi, Dinawi Samwel, Makiwa Handson, Rajab Rajab, Ezekiel Mleli, Neema Mwinyipembe na madereva Isaya Haruni, Juma Johari na Anderson Chiduli.

Shule hiyo ya Msingi Kidete inadaiwa kupokea ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwamo serikali, huku kampuni ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) Yep Merkezi, wakisaidia ujenzi wa vyoo vya shule.

Mwambambale katika utumishi wake wilayani Kilosa, amewahi kukutwa na matatizo mbalimbali ziliozoripotiwa na vyombo vya habari na kufikia kuomba radhi mbele ya aliyekuwa Rais, John Magufuli, kijiji cha Ilonga, baada ya kutuhumiwa kugawa shamba lililokuwa likigombewa na wananchi na mwekezaji.

Mei 19, 2020 alidaiwa kupeleka taarifa ya barua kwa wananchi kuwa mwekezaji Frank Palilo alikuwa akimiliki eneo la ardhi la ekari 1,600 badala ya 1,200 katika eneo la Ilonga, ambazo serikali ndio ilikuwa ikizitambua na alifanya hivyo bila kushirikisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wala Mkoa.

Pia alidaiwa kufanya hivyo bila kusubiri uamuzi wa timu iliyokuwa imeundwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ikilenga kufufua mipaka na mashamba yaliyokuwa yametelekezwa katika mkoa wa Morogoro.

Katika malalamiko ya wananchi kwa Rais, walilalamikia kukosa maeneo ya kulima baada ya mwekezaji kupewa eneo kubwa la ardhi, tofauti na eneo alilokuwa amenunua, huku wananchi wakiambulia ekari 145 na nusu tu.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilim, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Morogoro jana, kuhusu kuwakamata na kuwahoji watuhumiwa wanane akiwamo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Asajile Lucas Mwambambale, kutokana na tukio la wizi wa mabati 1,172 mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Bunge laagiza vigogo Geita washughulikiwe

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imetoa maagizo manne kwa Sekretarieti ya Mkoa wa Geita ikiwamo kuwachukulia hatua watumishi waliobainika kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya matumizi ya Sh. milioni 266 yasiyo na vielelezo.

Akizungumza maagizo hayo, ambayo kamati ilikuwa ikihoji fungu la 63 la sekretarieti hiyo kufuatia hoja za CAG za mwaka 2019/20, Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alisema hatua hizo zichukuliwe kwa kuwa fedha hizo zinaonekana zimeibwa kwa mujibu wa taarifa ya mkaguzi.

"Ofisa Masuhuli ahakikishe anawachukulia hatua na warudishe hizo fedha waliobainika kwenye ripoti ya CAG ndani ya kipindi cha mwaka huu wa fedha 2021/22," alisema.

Hasunga alisema malipo ya kiasi hicho hayakuwa na vielelezo vyovyote na walipoulizwa, walisema vielelezo vimepotea.

"Pia tumewaagiza kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kuwa imeonekana mikataba yao ya ununuzi haijazingatia sheria hiyo," alisema.

Kiongozi huyo wa kamati alisema kulikuwa na mkataba wa ujenzi wa Sh. milioni 792, lakini mkaguzi alipokwenda kupitia mkataba na kuangalia BOQ, ilionekana mkataba ulitakiwa uwe wa Sh. milioni 592, hivyo walisaini mkataba na kuzidisha Sh. milioni 200 kinyume cha maelekezo yalipopo kwenye BOQ.

"Kadhalika, kuna kuvunja mkataba wa jengo waliloamua kukarabati ambalo walipewa na Chama cha Ushirika cha Nyanza, waliamua kuanza kukarabati baadaye ushirika walipogawana jengo linaonekana bado ni la chama hicho kwa hiyo halijagawiwa serikalini na tayari walishatumia zaidi ya Sh. milioni 600 kukarabati jengo ambalo halikutolewa kwa kufuata taratibu za ushirika," alifafanua.

Alisema kamati pia, imeagiza kufuatiliwa kwa vifaa tiba na dawa katika Bohari ya Dawa (MSD), ili wananchi wapate huduma.

"Kampuni ya GGM ilitoa Sh. milioni 400 kwenda MSD, kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba lakini imeonekana hadi sasa MSD haijapeleka vifaa na dawa vyenye thamani ya Sh. milioni 149 kinyume cha mkataba na sekretarieti iliagiza ipelekewe vifaa, lakini hadi sasa havijapelekwa na fedha hazijarudishwa hadi leo," alisema.

# Raia wa kigeni mbaroni tuhuma kupata fedha kwa madini bandia

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia raia wa kigeni na wenzake wakidaiwa kujipatia fedha kwa kuuza madini bandia.

Watu hao ni miongoni mwa watuhumiwa 17 wanaoshikiliwa kwa madai ya kujihusisha na vitendo vya kihalifu vya jinai.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi (ACP) Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa hao walikutwa na madini bandia na mitambo ya kuyatengeneza.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wamekamatwa kupitia operesheni inayohusisha vikosi vya mbwa, farasi na askari.

Alisema Agosti 20, mwaka huu, Jeshi la Polisi liliwakamata watuhumiwa 13 akiwamo raia wa Afrika Kusini, Harold Martin (60) maarufu kwa jina la Pouwes na Christopher Robert (29) maarufu kama Manyanga mkazi wa Tabata Bima.

Alisema watuhumiwa hao wawili inadaiwa huwaongoza wenzake 11 kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu wa kuuza madini bandia na kwamba walikamatwa Agosti 20, mwaka huu saa 9:00 alasiri maeneo ya Mbezi Makonde.

Kwa mujibu wa Muliro, uchunguzi wa shauri hilo unakamilishwa kwa ushirikiano na vyombo vingine vya dola. Alisema watuhumiwa hao inadaiwa walikutwa na boksi nne zenye madini bandia zinazodhaniwa kuwa ni dhahabu, mitambo miwili inayodaiwa ni ya kuyeyushia madini, kifurushi kimoja cha madini bandia na vipande saba vya madini bandia.

Kamanda Muliro alitaja vingine kuwa ni hati za kusafiria tano na kwamba watuhumiwa hao hujifanya ni wafanyabiashara wa kimataifa na wamekutwa pia na magari sita ambayo wanaendelea kuyachunguza waliyokuwa wanayatumia kufanyia vitendo hivyo vya kitapeli.

Katika tukio la pili, Kamanda Muliro alisema wamewakamata watuhumiwa wanne wanaodaiwa kujihusisha na unyang'anyi wa pikipiki.

"Watuhumiwa hao ni Hizza Herbert (52) mkazi wa Tabata, Richard George (45) mkazi wa Buguruni, Arif Henry (21) mkazi wa Buguruni na Saad Mohamed (25) mkazi wa Mburahati. Watuhumiwa hawa walikamatwa na vielelezo vya pikipiki nne walizozipora maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, baadhi zimeshatambuliwa na wamiliki," alisema.

# Hoja 11 kero Muungano zaondolewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKAO cha pamoja cha kujadili changamoto za Muungano kati ya mawaziri wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zanzibar kimekubaliana kuondoa hoja 11 zilizokuwa kero.

Hatua hiyo inatokana na majadiliano yaliofanyika kwa pande mbili za Muungano katika kikao kilichofanyika Mjini Zanzibar kikiongozwa na Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akitoa taarifa kabla ya utiaji saini wa hoja hizo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ya Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alisema hoja hizo ni uvuvi katika ukanda wa bahari kuu, ajira kwa watumishi wa umma katika taasisi za Muungano na tozo ya miamala ya simu.

Hoja zingine ni mgawanyo wa mapato utokanao na msaada wa masuala ya kibajeti kwa asilimia 4.5 kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ukarabati wa Hospitali ya Mnazimmoja Zanzibar.

Hoja zingine ni mkataba wa mkopo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Wete hadi Chakechake Pemba, mkataba wa mkopo wa Bandari ya Mpigaduri Zanzibar, na hoja ya usimamizi ya ukokotaji na usimamizi wa kodi za mitandao ya simu unaofanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na hoja ya mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar.

Alisema kuondolewa kwa hoja hizo katika Muungano kutaleta faida kubwa kwa vizazi vya sasa na baadaye katika pande hizo mbili.

Alisema mafanikio mengine yatakayopatikana ni kuimarisha uchumi na kuondoa usumbufu kwa wananchi na kuendelea kushikamana, kushirikiana na kujenga umoja wao.

Pia, alisema kuondolewa kwa hoja hizo utakuwa mustakbali mzuri na alama ya kwanza katika kushughulikia hoja hizo tangu Muungano huo ulipoasisiwa mwaka 1964.

Naye Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Abdullah, alisema Muungano wa Tanzania ni nguzo muhimu kwa taifa nao kusainiwa kwa makubaliano ya hati hizo ni matukio chanya ya vikao kati ya Serikali ya SMT na SMZ.

"Leo kusainiwa kwa hati za makubaliano haya kuna faida kubwa na itasaidia kuondoa migongano, manung'uniko na malalamiko kwa vizazi vya sasa na baadaye na kupata maendeleo," alisema.

Alisema makubaliano hayo yatawajengea imani wananchi kutatua changamoto zinazowakabili ambazo zilikuwa zikiwakwaza kabla ya hoja hizo kuondolewa katika masuala ya Muungano.

Makamu wa pili alisema: "Kuna baadhi ya watu walitaka Muungano huu uvunjike kwa madai ya upande mmoja wa kufanya maamuzi bila ya makubaliano, lakini ilani ya CCM inasisitiza kuimarisha Muungano huo."

Kwa upande wake Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema kusainiwa na kukubaliwa kwa hoja hizo wananchi wataendelea kuendesha shughuli zao kwa amani na utulivu.

Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, alisema hoja mbili ambazo hazijatiwa saini jana kati ya 11 ni za kiutendaji ambazo hazihitaji hati.

Hoja hizo ni uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya amana na uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kikodi.

Alisema tukio la kusaini hati ya makubaliano ya hoja za Muungano lengo lake ni kuimarisha kwa dhati Muungano huo na kuulinda.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akikagua usafi katika vyoo vya Shule ya Sekondari ya Ng'ang'ange, wakati akiwa katika ziara ya kikazi, wilayani Kilolo, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Rungwe sasa aibukia chanjo ya corona

**Donald Lukele,** TUDARCo

MWENYEKITI wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashim Rungwe, amezungumzia mvutano uliojitokeza kati ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, na Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, akimtetea waziri huyo kuwa hahusiki na mapendekezo ya Watanzania kuchanjwa chanjo ya corona.

Rungwe aliyekuwa mmoja wa wagombea wa nafasi ya Kiti cha Rais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliopita, akitamba na ahadi yake ya ubwabwa shuleni, amesema waliopendekeza wananchi wachanjwe ni kamati iliyoundwa na Rais Samia Suluhu.

Akizungumza na Nipashe Kinondoni, Dar es Salaam jana Rungwe alisema wanaombebesha lawama Waziri Dorothy kuhusu suala la chanjo hawako sahihi kwa kuwa kamati iliyoundwa na Rais Samia ndiyo iliyoishauri serikali nini kifanyike kupambana na corona.

Alisema kuletwa kwa chanjo ya corona nchini ni moja ya mapendekezo yaliyotolewa na kamati hiyo.

"Baada ya serikali kujiridhisha juu ya usalama na ubora wa chanjo, sasa inatekeleza wajibu wake," alisema.

Rungwe alisema anaamini kuletwa kwa chanjo hiyo ni neema kwa taifa kwa kuwa nchi imepata mwangaza wa kukabiliana na ugonjwa huo na wananchi wanapaswa kujitokeza kwa wingi kupata chanjo.

"Mimi nimepata chanjo tayari, hata watu wangu wa karibu katika chama chetu wamepata chanjo. Dhumuni ni kuhakikisha tunapata kinga ya ugonjwa huu hatari, hivyo ninawaomba Watanzania wote wajitokeze katika vituo vya afya kuhakikisha wanapata chanjo.

"Hawa wanaoipotohsa jamii, mimi naweza kuwaita ni washamba na wana mawazo ya kizamani. Mataifa mengi sasa wanahimiza watu wao kupata chanjo. Sisi tumeipata kwa nini tusichanjwe?" Rungwe alihoji.

Alisema kama watu hao wanaona chanjo haifai basi serikali iwape eneo waanzishe viwanda vya kutengeneza chanjo zao ili wawaletee wananchi chanjo sahihi na si kuishia kuongea tu.

**TOZO ZA MIAMALA**

Akizungumzia tozo za miamala ya simu na utaratibu mpya wa kulipa Kodi ya Majengo kwa LUKU, Rungwe alisema serikali inawabebesha mzigo wananchi wenye maisha ya chini.

Kwa kutambua hilo, aliishauri serikali kutafuta njia mbadala ya kuimarisha makusanyo yake bila kuumiza Watanzania.

Alisema zipo njia mbadala za kupandisha uchumi wa nchi kama kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa serikali kama vile safari na kubana kodi kwa bidhaa zinazoingia nchini ili kukusanya mapato mengi zaidi.

**KATIBA MPYA**

Kuhusu hoja ya kudai Katiba Mpya inayotiliwa mkazo na baadhi ya vyama vya siasa nchini vikiwamo CUF, CHADEMA na ACT-Wazalendo, Rungwe alisema serikali iliyopo ifungue milango na kukaa mezani na vyama vya upinzani ili kujadili masuala yanayohusu suala hilo.

Alisisitiza kuwa kwa kufanya hivyo, watahakikisha katiba hiyo inatungwa kwa manufa ya nchi kwa kujenga demokrasia safi na usawa katika nyanja za kisiasa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ya uchaguzi muhimu iboreshwe

**MWISHONI** mwa wiki, Rais Samia Suluhu Hassan, alipokea Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 iliyowasilishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), alisema inatakiwa kuangalia upya sheria ili zisitumike kuwanyima watu haki wakati wa uchaguzi.

Haki hizo ni kukosea au makosa mengine kwenye fomu za kuomba kuteuliwa kugombea, kauli ambayo ililipigiwa makofi na washiriki wa mkutano, ambao wengi walikuwa kutoka vyama vilivyoshiriki uchaguzi mkuu mwaka jana.

Tunampongeza Rais Samia kwa kuliona hilo na iwapo sheria hizo zitafumuliwa, ni vyema ushiriki wa wadau wote ukawapo, ili kuondoa malalamiko katika kujenga demokrasia nchini. Yapo mengi yanayolalamikiwa kwenye uchaguzi kila unapofanyika, na mwisho wengi huishia kuona kuwa ili mchakato huo usiwe na malalamiko, ni muhimu kuwa na Katiba mpya.

Mwaka 2014, Bunge Maalum la katiba lilikamilisha mchakato wa Katiba mpya ambao ulianzia kwenye ukusanyaji wa maoni ya wananchi na kupata rasimu chini ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Warioba.

Katiba inayopendekezwa ilipaswa kwenda kwenye hatua ya mwisho ya kurudishwa kwa wananchi kwa ajili ya kura ya maoni, lakini haukufika mwisho hasa baada ya kuwapo mvutano kati ya wajumbe ulioonekana kusababishwa na tofauti itikadi za vyama.

Baada ya mchakato huo kukwama kulikuwa na ahadi ya kufanya marekebisho ya katiba iliyopo ya mwaka 1977 ili kuweka mazingira bora ya uchaguzi mkuu wa 2015.

Mambo yaliyotakiwa kufanyiwa marekebisho kwenye Katiba ya sasa ni kuruhusu kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi, kuwaruhusu wagombea binafsi, kuruhusu matokeo ya uchaguzi wa rais kupingwa mahakamani na anayeshinda urais kutakiwa kupata kura zaidi ya asilimia 50.

Kata hivyo, serikali ya Jakaya Kikwete haikuitekeleza ahadi hiyo. Rais aliyemfuatia, Hayati John Magufuli, alisema suala la katiba mpya halikuwa ajenda yake kwa wakati huo, lakini Rais Samia ameahidi kulishughulikia, ingawa ameomba apewe muda kwanza aisimamishe nchi.

Vyama vya upinzani na wadau wengine wameendelea kupaza sauti kudai Katiba mpya, kutokana katiba ya sasa hasa Sheria ya Uchaguzi kuonekana ni kikwazo kikubwa kwenye mchakato wa uchaguzi.


Kwa mfano, Zambia iliyofanya uchaguzi Agosti 12, mwaka huu, imeonyesha kwamba kuwapo kwa mazingira mazuri ikiwamo katiba na sheria nzuri ndiyo dawa ya kutokuwapo malalamiko na uchaguzi kuwa huru na haki pamoja na kuaminika.

Sheria yao imeruhusu mgombea binafsi na wapo ambao walishindwa kwenye kura za maoni ndani ya vyama vyao na na kuendelea na ndoto zao za uongozi wa kisiasa kama wagombea binafsi. Lakini inaruhusu mchakato wa kupata makamishna wa tume ya uchaguzi ambao ni wa wazi na hauingiliwi na yeyote kiasi kwamba hata ikitangaza matokeo yanaaminika.

Pia, Katiba yao inataka mshindi kuwa na kura zaidi ya asilimia 50 na sheria inaruhusiwa matokeo ya rais kupingwa mahakamani baada ya tume kuyatangaza. Mahakama inaweza kuamuru kura kurudiwa kuhesabiwa au kufuta uchaguzi kutegemea na ushahidi.

Ni muhimu maoni ya wadau wa uchaguzi kusikilizwa na kushughulikia kasoro zote ambazo zinazua shaka ya mchakato hadi kutangazwa kwa mshindi. Tunatarajia kuona viongozi wetu wanayachukua na kuyafanyia kazi mazuri yote yalioonekana katika uchaguzi wa Zambia ili nchi yetu iwe na uchaguzi mzuri, huru na haki pamoja na kuaminiwa na wadau wa uchaguzi nje na ndani ya Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Rais ameahidi kuboresha uchaguzi mkuu ujao, tulieni

Na Miki Tasseni

**MSUKUMO** wa kuwapo mkutano kati ya Rais Samia Suluhu Hassan na vyama vya siasa huenda ukapungua nguvu baada ya Rais kupokea taarifa ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana, na kutoa maagiza ya kufanyiwa kazi.

Kinachofanya pengine wanasiasa kupoa moto ni aliyoyasema kuhusiana na taarifa hiyo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, 2020.

Licha ya kwamba alitumia muda mwingi zaidi kugusia yaliyotajwa ndani ya ripoti hiyo na katika maongezi yake ya ziada alihimiza ushiriki wa wanawake kwani wapo wachache wanaoteuliwa kwa nafasi za kugombea, kuanzia ile ya urais, ubunge na udiwani.

Hilo lilitazamiwa lakini halikuwa linawasumbua wengi kwani ni suala la muda mrefu sasa na kila mara ajenda ya 50/50 imekuwa ikipewa msukumo mpya kwenye masuala ya uchaguzi, au kuelekea kwenye uchaguzi.

Kilichokuwa kinangojewa kwa hamu zaidi katika hotuba yake ni hisia zake kuhusu uchaguzi ulivyoendeshwa, kwamba ni kwa kiasi gani angefaulu kuhuisha uenyekiti wake wa chama tawala na namna uchaguzi ulivyoendeshwa.

Wengi walihofia au labda kutazamia kuwa asingezungumzia suala hilo, na kwa sehemu kubwa ya maongezi yake alilenga kupongeza kazi iliyofanywa na Tume ya Uchaguzi (NEC), hasa kuzungumzia ushindi wa zaidi ya asilimia 86 tofauti na asilimia 62.5 uliofikiwa mwaka 2015.

Itakumbukwa kuwa hata mwaka 1995 wakati Rais mstaafu Julius Nyerere, alipoipigia kampeni CCM, haikuvuka wastani wa 62.5 wa kura.

Wakati ule, mtaalamu wa siasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Gaspar Munishi, alisema CCM ingepata asilimia 70 ya kura majimbo ya uchaguzi vijijini.

Ndivyo ilivyokuwa, wakati inafahamika kuwa CCM inapata kura nyingi zaidi vijijini kuliko mijini, lakini miaka ya karibuni upinzani umefaulu kujijenga hata vijijini, hivyo kushinda baadhi ya majimbo ya vijijini uchaguzi mkuu 2015.

Ina maana hapakuwa na uwezekano wowote ule wa CCM kufikia asilimia 86 ya kura katika uchaguzi ulioendeshwa kwa haki, uwazi na ukweli na kukubalika inavyotakiwa.

Uendeshaji wa uchaguzi mkuu uliopita umekuwa kigezo kimojawapo muhimu katika madai ya jumla la kupatikana kwa katiba mpya kwa upande wa CHADEMA na hivyo uwepo wa hatari ya kuvuruga utulivu endapo mvutano unaoendelea hautapatiwa ufumbuzi.

Isitoshe Rais Samia amekuwa akipata shinikizo kutoka nchi tofauti hasa Ulaya na Marekani, ambako hivi majuzi Ikulu ilitembelewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Victoria Nuland.

Licha ya kuwapo masuala kadhaa muhimu kwa mfano hali ya Msumbiji, ushirikiano na China, biashara na Marekani, bado suala la demokrasia lilifuatiliwa kwa karibu na vyombo vya habari kuhusiana na majadiliano hayo.

Taarifa za hivi karibuni zilisema kuwa CHADEMA ilikataa mwito wa kuwepo ikulu wakati wa kutolewa kwa ripoti ya Tume ya Uchaguzi, jambo ambalo halikushangaza, hasa kutokana na mwenyekiti wake kuwa rumande wa mashtaka ambayo hayana dhamana.

Hata hivyo, kwa vile kuna ushindani kati ya vyama vya siasa na siyo kati yao na chama tawala vingine vilikuwapo na kushangilia Rais Samia alipogusia kilichowakera uchaguzi mkuu uliopita.

Ni kuondoa majina ya wagombea kwa madai ya kukosea baadhi ya herufi au ya vyama vyao, jambo ambalo Rais Samia alilitaja lilivyo bila kulitilia shaka.

Kwa hatua hiyo inachukuliwa kuwa amedhihirisha uwajibikaji aliposema 'tuliwapiga pini' na maeneo mengi wagombea wa CCM wakapita bila kupingwa. Hakuikosoa NEC moja kwa moja ila alitaka waboreshe wanachokifanya katika uchaguzi ujao. Ina maana waache tabia hiyo au alitaka kusema inatosha.

## Mtaka atoa elimu kuepusha watumishi kuibiwa wakistaafu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amekitaka Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) kuwa na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wake kabla ya kustaafu.

Amesema hatua hiyo itawaepusha kuangukia katika mikono ya matapeli pindi wanapopata mafao yao.

Pia ameitaka TALGWU kuacha kuwa chama cha uanaharakati badala yake itetee na kusimamia masuala ya msingi ya wanachama wake.

Mtaka alisema hayo jana alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa TALGWU, ambao pamoja na mambo mengine unalenga kufanya uchaguzi mkuu wa viongozi wake.

Mtaka alisema siku hizi kumekuwa na matapeli wengi wa mitandao na taasisi nyingi za mikopo ambazo watumishi wengi hujikita kwenda kukopa na matokeo yake wanakuja kulipa wupokuwa na mafao yao kipindi wanapostaafu.

Kutokana na ongezeko la wimbi hilo, alishauri elimu itolewe ya namna ya kutumia mafao yao kwa wastaafu.

"TALGWU mnapaswa kulianza hilo mapema, ili watumishi wanapostaafu wanakuwa na elimu hiyo kichwani mwao," alisema Mtaka.

Aliwataka kuwa na malengo yanayoishi ikiwamo kuweka vitega uchumi ambavyo vitawasaidia katika kujiendesha na kusisitiza kulinda heshima ya chama hicho na kutojiingiza kwenye masuala ya uanaharakati. Alisema viongozi mnapaswa kuwa makini kulinda chama, ili kiwe mfano wa kuigwa.

"Wito wangu kwenu tusimamie maadili ya watumishi tuwatetee kwenye mambo ya msingi hata kwenye gharama za kesi fanyeni zile zenye mantiki, ili muache alama nzuri, sio mtu kalewa kasasabisha kesi nayo mnaitetea," alisema Mtaka.

Aidha, Mtaka alitoa wito wa kuwekeza jijini Dodoma kwa kuwa kuna fursa nyingi baada ya serikali kuhamia Dodoma.



Abiria wakiwa wamejipanga foleni wakisubiri daladala kwenye kituo cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, ambapo wameweka utaratibu huo ili kuepusha usumbufu wa kusukumana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ACT - Wazalendo yabaini tatizo elimu chanjo corona

**Na Donald Lukele,** TUDARCo

CHAMA cha ACT-Wazalendo kupitia ngome yake ya vijana, kimeishauri serikali kuhakikisha inaongeza nguvu katika utoaji wa elimu kwa wananchi ili wahamasike na kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19, hivyo kutimiza kikamilifu dhamira ya kukabiliana na ugonjwa huo unaotikisa dunia.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano kwa Umma Ngome ya ACT-Wazalendo, Julius Massabo, alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu ugonjwa huo, akilalamika kuwa jamii bado haijapata elimu ya kutosha juu ya chanjo hiyo.

Kutokana na dosari hiyo, Massabo alisema chama chao kinaamini ndiyo sababu ya wananchi wengi kushindwa kujitokeza kupata chanjo hiyo.

"Tumeona serikali ikitoa elimu kwenye chanjo za surua, chanjo za polio, tumeona kampeni nyingi zikifanywa na Wizara ya Afya kuhamasisha watu wajihusishe kwenye masuala ya afya lakini kwenye corona imekuwa tofauti," alisema.

Massabo alisema bado jamii ina maswali mengi na hawana taaluma ya kutosha kuhusiana na chanjo, hivyo inapotoshwa kwa sababu haijaelezwa kwa kina na vya kutosha chanjo ni kitu gani, inafanya kazi gani na ipo kwa manufaa gani, hivyo kupelekea malengo ya Wizara ya Afya dhidi ya kutokomeza janga hili kutofikiwa kwa wakati.

Alisema serikali haina budi kuweka mikakati na iboreshe zaidi njia za kufikisha elimu kote nchini kwa kushirikiana na taasisi na wadau mbalimbali wa afya ili hata Watanzania walioko vijijini wapate elimu ya kutosha juu ya chanjo hiyo.

Massabo alisema chama chao kimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha serikali inaleta chanjo ili watu wapate kinga dhidi ya ugonjwa huo.

Serikali ilianza rasmi utoaji wa chanjo hiyo kitaifa Agosti 3 mwaka huu, uchanjaji huo ukizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan aliyechanja na kusisitiza chanjo ya UVIKO-19 inatolewa kwa hiari bila malipo.

***Imeandaliwa na Donald Lukele, TUDARCo na Mary Geofrey**

# Waliopatiwa chanjo ya corona wafika 261,000

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imesema takribani Watanzania 261,000 wameshapata chanjo ya UVIKO-19 aina ya Johnson & Johnson na wanaendelea vizuri kiafya.

Waziri wake, Dk. Dorothy Gwajima, aliyabainisha hayo jana jijini Dar es Salaam aliposhiriki dua ya kuukaribisha mwaka mpya wa Kiislamu 1443 Hajiria, iliyoandaliwa na Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA).

Dua hiyo pia ilikuwa inalenga kuliombea taifa na Rais Samia Suluhu Hassan na kumwomba Mungu aliepushe taifa na maradhi ya UVIKO-19.

Dk. Dorothy alisema licha ya idadi hiyo ya Watanzania waliochanja, idadi kubwa ni wanaume zaidi ya asilimia 50 kulinganisha na wanawake ambao wameonekana kuwa nyuma.

"Waliochanja wapo wanaendelea na shughuli zao kama mimi tangu nimechanjwa kazi inaendelea, kwanza ninajiamini, sina shaka yoyote. Mume wangu amechanjwa, majirani zetu wamechanjwa, wote waliochanjwa, wakuu wa wilaya, mikoa na Watanzania wengi mpaka vijijini tunawashukuru sana," alisema Dk. Dorothy.

Kuhusu elimu ya UVIKO- 19 kuwafikia watu, alisema itaendelea kutolewa kwa wengi na itawafikia wale ambao masikio yao yameamua kusikia isipokuwa wale ambao hawataki kusikia na serikali haiwalazimishi.

"Tunawaombea kwa mwenyezi Mungu elimu iwafikie lakini kama sikio lako limejaliwa umauti, hawa nao wenyewe tunawapa heshima yao.

"Elimu kama haijakufikia, itafute elimu, yatafute maarifa kwa watu sahihi. Kumezuka utaratibu wa watu wasio waadilifu, kuzikata taarifa fupi fupi za elimu inayolewa ili zishushe heshima za watu na kuleta taharuki.

"Ndugu zangu ukipata elimu kabla ya kuanza kushangaa, waulize waliotuma vipande wakupe kipande chote cha taarifa kwa sababu watu wamejipanga kupotosha mambo mengi na faida msiipate," alisisitiza Dk. Dorothy.

Dk. Dorothy alisema serikali inaendelea kuhimiza umuhimu wa chanjo ili Watanzania wanaohitaji huduma hiyo waipate kwa wakati.

Alisema wanawake ni zaidi ya asilimia 51 kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi, lakini hawajajitokeza wengi kupata chanjo hivyo watatumia utaratibu wa kuwafikia katika maeneo walipo.

Alisema kwa nchi zinazochelewa kuchanja ugonjwa wa UVIKO-19 unashuka hadi kwa watoto na hivyo kunaweza kusababisha watoto kupata maambukizi.

Waziri huyo aliwahimiza Watanzania kujikinga kwa kupata chanjo ili kulikinga kundi la watoto wadogo, kuokoa maisha ya watu na wanaogua ugonjwa huo wasishindwe kupumua.

Kuhusu mikopo ya wanawake na vijana inayotolewa katika halmashauri mbalimbali nchini, Dk. Dorothy alisema fedha zinatoka lakini mwitikio ni mdogo kwa wakopaji.

"Tunatoa mikopo lakini fedha zinarudi, sasa ninaomba tushikirikiane hatua kwa hatua ili watu wapate mikopo na fedha zisirudi tena serikalini," alisema Dk. Dorothy.

Alisema lengo la serikali ni kuchanja Watanzania milioni 35 sawa na asilimia 60 kwa kutanguliza makundi ya kipaumbele kama watoa huduma za afya, wazee na watu waliopo katika hatari ya kupata maambuki.

Serikali ilipokea chanjo dozi 1,058,400 za UVIKO-19 aina ya Johnson & Johnson Julai mwaka huu kutoka Serikali ya Marekani kupitia mpango wake wa Covax, unaolenga kusaidia nchi zinazoendelea katika kukabiliana na janga hilo.

# Wajawazito, watoto wadaiwa kutozwa fedha kupata matibabu vituo vya afya

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

LICHA ya serikali kuweka sera kwamba wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kupatiwa huduma ya matibabu bure, katika Halmashauri ya Mji wa Bunda wamekuwa wakitozwa fedha katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma ya afya.

Hayo yalisemwa juzi na baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo kwenye mkutano wa mwaka wa fedha wa 2020/21 wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika ukumbi wa halmashauri mji hapo.

Flavian Nyamageko, Diwani wa Bunda Stoo, Emmanuel Malibwa wa Nyamakokoto na Mohonda Nyahimbo wa Kabarimu, walitoa madai hayo wakati wakichangia hoja.

"Sera ya serikali inasema wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano watibiwe bure. Sasa je, mwenyekiti ninataka kujua mbona wanapokwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wamekuwa wakiambiwa walipie au wakanunue dawa hili likoje?" Alihoji Nyamageko.

"Mheshimiwa mwenyekiti mimi ni mmoja wa wahanga (waathirika), mke wangu alikwenda hospitalini akaambiwa atoe pesa. Mpaka tulipotoa pesa ndipo akapewa huduma. Hii sera ya serikali mbona haifuatwi?" Alisema Malibwa.

Akijibu hoja hiyo, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Dk. Richard Majahasi, alisema changamoto hiyo inayakumba makundi hayo baada ya kukuta vifaa tiba na dawa zimekwisha, hivyo kulazimika kununua kwenye maduka ya serikali yaliyoko kwenye vituo husika kwa bei nafuu.

"Changamoto hiyo huwa inatokea pale tu dawa na vifaa tiba vinapokuwa havipo kituoni, lakini tumekuwa tukiwaambia wanunue kwenye maduka ya serikali kwa kuuziwa kwa bei nafuu," alisema.

Hata hivyo, madiwani hawakuridhika na majibu hayo na kusema jukumu la Bohari ya Kuu ya Dawa (MSD) kuleta dawa za kutosha kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya na kwamba hiyo ni sawa na kuchonganisha serikali na wananchi kwa kuwa sera inatamka wazi kupata huduma bure.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Emmanuel Mkongo, alisema suala hilo ni nyeti na wamelichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi, ili kuhakikisha wanaiondoa kero hiyo.




Meneja Mwandamizi wa Uhusiano kwa wajasiriamali wadogo kutoka Benki ya CRDB, Seuri Meijo, akitoa mada kwa wajasiriamali katika Tamasha la Kizimkazi visiwani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni akidaiwa kukutwa na risasi 25

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamshikilia Yunus Dossa (40) mkazi wa Lugoba, Chalinze wilayani Bagamoyo kwa tuhuma za kukutwa na risasi 25 zenye ukubwa wa milimita 75.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema katika taarifa yake jana kwamba mtuhumiwa huyo alikutwa na risasi hizo ambazo alikuwa amezihifadhi chumbani kwake.

Wankyo alisema katika upekuzi, Dossa alikutwa pia na mihuri mitatu ukiwamo wa Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Chalinze, mhuri wa Mtendaji wa Kijiji cha Malivundo na wa Mwenyekiti wa Kitongoji cha Malivundo.

Alisema upelelezi kuhusiana na tuhuma za mtuhumiwa huyo ambaye ni mjasiriamali unaendelea na ukikamilika atafikishwa mahakamani.

Katika tukio lingine, watu wawili wamekamatwa kwa tuhuma za kukutwa wakimiliki silaha aina ya gobore kinyume cha sheria.

Kamanda Wankyo alisema watuhumiwa hao walikamatwa Agosti 13, mwaka huu, majira ya saa 6:00 usiku huko Kimange katika halmashauri ya Chalinze na wilaya ya Kipolisi ya Chalinze.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Shabani Bakari (40) mkazi wa Kimange na Chambuli Kitwana (42) mkazi wa Miono, wote wakiwa na silaha hizo wanazimiliki bila vibali.

Kamanda pia alisema wako watuhumiwa watatu ambao wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kuvunja nyumba na kuiba mali zinazodaiwa ni za Kampuni ya Yep Merkez huko Kinzagu Lugoba.

Wankyo alisema polisi baada ya kupata taarifa, walianza msako na kuwakamata watuhumiwa siku sita baada ya kutokea tukio hilo.

Aliwataja watuhumiwa kuwa ni Idrisa Bakari (34), Maenga Sekeni (36) na Zuber Luweza (36) wote wakazi wa kinzagu Lugoba.

Alisema watuhumiwa hao baada ya kukamatwa walikutwa na nyaya tatu za jenereta, vipande sita vya meza za kichina na magodoro mawili ambavyo vinadaiwa vilikuwa katika stoo ya ujenzi ya kampuni hiyo.

# Taasisi yatamani watumishi NEC kila wilaya nchini

**Na Sabato Kasika**

TAASISI ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), imesema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ikiwa na watendaji wake hadi ngazi ya halmashauri, kasoro ambazo hujitokeza mara kwa mara katika uchaguzi zitapungua.

Moja ya kasoro hizo, zimetajwa na CEGODETA ni tuhuma za kuwapo kwa baadhi ya mawakala wa vyama kunyimwa nakala za viapo kutokana na kwamba baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi hiyo ni makada.

Hayo yalisemwa jana na mwenyekiti wa taifa wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, alipozungumzia mapendekezo yaliyotolewa na tume hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan ilipokabidhi ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"CEGODETA tunajua kwamba uchaguzi huwa unakumbwa na kasoro nyingi ikiwamo ya baadhi ya mawakala kunyimwa viapo, hiyo inatokana na kwamba baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri ni makada," alisema Ngawaiya.

Alisema, wao kama watu wa utawala bora, wanaamini kwamba tume ikiwa na watumishi wake kuanzia ngazi ya chini, hakutakuwa na kasoro zilisizo za lazima ambazo wakati mwingine husababishwa na wasimamizi.

"Wengine husababisha kasoro zisizo za lazima katika uchaguzi kwa ajili ya kulinda vibarua vyao na pia ni makada, lakini kama tume itakuwa na watumishi wake, angalau unafuu unaweza kuwapo," alisema.

Aliongeza kuwa njia hiyo pia itawafanya wananchi wapate viongozi wanaowataka na hata kusaidia kuwaletea maendeleo, badala ya kuchaguliwa na wasimamizi kutoka halmashauri.

"Sisi watu wa utawala bora tunaipongeza tume kwa kuchukua maoni ya wadau, ambao wamependekeza kuwapo kwa watumishi wake kuanzia ngazi ya halmashauri, kwani huko ndiko hutokea kasoro nyingi," alisema.

Aidha, alisema, CEGODETA inapendekeza kutumika kwa mfumo wa TEHAMA katika uchaguzi, ambao utasaidia kila jambo kufanyika kwa uwazi ili kila Mtanzania aweze kuona kura yake.

NEC itoa mapendekezo kadhaa yaliyotolewa na wadau mbalimbali nchini, kwa lengo la kusaidia kuboresha uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025 ilipokuwa ikikabidhi ripoti ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Miongoni mwake kuona uwezekano wa NEC kuwa na watendaji wake hadi kwenye ngazi ya halmashauri na pia serikali kutoa fedha kwa ajili ya asasi za kiraia zinazotoa elimu ya mpigakura. Mengine ni kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura 292 pamoja na kutaka uchaguzi wa serikali za mitaa kusimamiwa na mamlaka moja.

HABARI KITAIFA

# Wenye ulemavu wampa tuzo Samia

**Na Beatrice Shayo**

UONGOZI wa Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Viziwi Tanzania (KISUVITA), umempa tuzo Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kutambua mchango wake katika kuhakikisha haki na usawa wa fursa kwa watu wenye ulemavu nchini.

Walisema wanamtambua Rais Samia pia kutokana na kuwawezesha kufanikiwa kushiriki mashindano ya kidunia ya mitindo na urembo Moscow nchini Urusi.

Tuzo hiyo imewasilishwa na kupokelewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka kwa niaba ya Rais Samia.

Wakati wa makabidhiano hayo Katibu Mtendaji wa kituo hicho, Habibu Mborobe, alisema wanampongeza Rais Samia kwa uongozi mahiri unaowashirikisha kuwa jumuisha na kuwathamini watu wenye ulemavu.

"Kwanza tunamshukuru kwa kuwezesha safari yetu ya kwenda kushiriki mashindano ya kidunia ya mitindo na urembo nchini Urusi ambako tulifanikiwa kushika nafasi ya kwanza. Ushindi huo umetupa heshima ya kuwa waandaaji na wenyeji wa mashindano kama hayo kwa kanda hii ya Afrika yatakayoanza kuanzia Septemba 29 hadi Oktoba 2, mwaka huu," alisema na kuongeza;

"Tunamshukuru na kumpongeza kwa serikali anayoiongoza kutoa fursa ya mikopo isiyo na riba itokanayo na asilimia mbili ya mapato ya ndani ya halmashauri, ambayo sisi wenye ulemavu tunanufaika nayo," alisema.

"Pia tunamshukuru kwa kuendelea kuhakikisha vyombo mbalimbali vya habari kuwa na wataalamu wa lugha za alama ili nasi tuweze kupata haki yetu ya kupata habari."

Ameiomba CCM iwasaidie kwa kuwa wakikosa kuungwa mkono na jamii zikiwamo kampuni za kibiashara kutoa udhamini kwa mashindano mbalimbali wanayoandaa au kushiriki.

Shaka alisema hawana tofauti na watu wenye kusikia kwa kuwa hata wao wanatumia bidhaa zote zinazozalishwa na kampuni hizo.

Akizungumza na ujumbe huo Shaka alisema, CCM itahakikisha watu wenye ulemavu wanashirikishwa, wanaheshimiwa, wanathaminiwa na wanajumuishwa katika mipango na programu mbalimbali za maendeleo ya nchi na serikali.

Alisema bajeti ya serikali ya mwaka 2021/22 imetenga takribani Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa visaidizi kwa watu wenye ulemavu kwenye shule zote nchini. Kwa mujibu wa Shaka, serikali imeendelea kuhimiza wataalamu wa lugha za alama kuwapo kwenye kila tukio ambalo umma unafuatilia ili kuwapa haki watu wenye ulemavu wa uziwi kupata habari.

Alisema CCM itaendelea kutoa msukumo kwa serikali kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaonufaika na mikopo isiyo na riba itokanayo na asilimia mbili za halmashauri bila vikwazo vyovyote.

Aliwashukuru KISUVITA kwa kumpa tuzo Rais Samia ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wake kwa watu wenye ulemavu nchini.

# Faini mil.1.5/- ununuzi bidhaa bila kudai risiti

**Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imewaonya wananchi wanaonunua bidhaa mbalimbali na kutodai risiti sahihi za kielektroniki huku ikionya kuwa wakikamatwa watakabiliwa na adhabu ya faini ya kati ya Sh. 30,000 hadi Sh. milioni 1.5.

TRA pia imesema wafanyabiashara wasiotoa risiti sahihi kwa wateja, watatozwa faini ya kati ya Sh. milioni 3 hadi Sh. milioni 4.5.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mwanza, Joseph Mtandika, alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa Julai, mwaka huu.

Mtandika alisema moja ya maeneo wanayopata shida katika ukusanyaji wa mapato ya serikali ni pamoja na kuwapo matumizi madogo ya mashine za kielekroniki, kwa ajili ya kutolea risiti kwa watu wanaonunua bidhaa mbalimbali.

"Matumizi hafifu ya mashine za kielektroniki kwa wafanyabiashara wameendelea kukwepa kutoa risiti za kielektroniki, ambazo zinasaidia kuweka kumbukumbu sahihi za ulipaji wa kodi ya serikali," alisema.

Alisema tatizo lingine walokutana nalo katika ukusanyaji wa mapato ni baadhi ya wanunuzi ambao wakinunua bidhaa hawadai risiti za kielektroniki na kwamba uelewa kwa wafanyabiashara bado ni mdogo katika kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

Hata hivyo, alisema katika kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa kipindi hiki, wameendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanapokutana nao katika mazingira tofauti pamoja na weledi wa wafanyakazi wao.

Kuhusu vyanzo vipya vya mapato, alisema ni pamoja na kodi ya zuio ambayo ni kwa mazao ya kilimo na mazao ya ziwani.

Alisema serikali imeanzisha kodi ya zuio ambayo ni asilimia mbili kwa mazao mbalimbali yanayozalishwa hapa nchini na ilianza kutozwa hapa nchini Julai 7, mwaka huu.

Kadhalika, alisema kwa upande wa kodi za ndani kwa Julai, walivuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kutoka Sh. bilioni 11.2 hadi Sh. Bilioni 11.5 sawa na asilimia 103.

"Kwa upande wa kodi ya forodha mwezi wa saba tulipanga kukusanya Sh. bilioni 4.515 na tulikusanya Sh. bilioni 5.969 sawa na asilimia 132," alisema.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kutunza kumbukumbu ya ununuzi na mauzo kwa kuwa itawasaidia kutengeneza hesabu zao kwa usahihi pia watakuwa na uwezo wa kupata mikopo katika taasisi za kifedha.



Wakazi wa Buguruni Chama, jijini Dar es Salaam wakichangia damu katika tukio lililoandaliwa na Bima ya Assemble kwa kushirikiana na Taasisi ya Damu Salama, kusaidia wahitaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bima Assemble, Damu Salama zachangia damu, kutoa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bima ya AAR na Taasisi ya Damu Salama zimeshirikiana kuchangia damu katika eneo la Buguruni-Chama jijini Dar es Salaam, ikiwa kama sehemu ya kujitolea kwa jamii katika kusaidia wahitaji wa damu salama nchini.

Taasisi hizo ambazo ni wadau wa sekta ya afya nchini, pia zilitoa huduma ya kupima afya za wakazi wa eneo hilo bure na kutoa huduma nyingine za kitabibu ikiwa ni pamoja na ushauri wa kitaalam kuhusu afya.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Mkuu wa kitengo cha mauzo na biashara wa Kampuni ya Bima ya Assemble, Hamida Rashid alisema kuwa, hatua hiyo ni sehemu ya utamaduni wa taasisi hizo wa kujali afya ya jamii na kushiriki kwa vitendo kuboresha na kulinda maisha ya jamii.

"Tukiwa kama wadau muhimu katika sekta ya afya, tumeonelea ni vyema kushiriki katika utoaji wa damu kwa kushirikiana na Damu Salama katika kuokoa maisha ya wanajamii wenye uhitaji sambamba na kuunga mkono juhudi za serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, za kupunguza vifo vitokanavyo na upungufu wa damu," alisema Rashidi.

"Tunafahamu mahitaji makubwa ya damu salama na ni jukumu letu, ndiyo sababu kampuni yetu ya Bima ya Assemble kwa kushirikiana na wadau wenzetu (NBTS) tumeonelea tushiriki kikamilifu katika utoaji wa damu," aliongeza.

Aidha, alisema taasisi hizo zimetoa huduma nyingine za afya ikiwamo ushauri wa kitabibu kwa wakazi wa Mombasa-Ukonga kwani wanaamini kuwa jamii inapaswa kupata elimu ya kutosha ya jinsi ya kujikinga na magonjwa na kuimarisha afya zao, ili kupunguza idadi ya watu wanaosumbuliwa na magonjwa yatokanayo na kutozingatia au kutofahamu masuala ya msingi ya kuimarisha afya zao.

Mtaalamu mwelekezi wa uchangiaji damu kutoka Damu Salama, Mariam Juma, alisema kuwa pamoja na kuchangia damu, taasisi hizo zimetumia fursa hiyo kutoa elimu kwa umma kuhusu namna bora ya kuimarisha afya zao, faida ya kuchangia damu na kuhuisha usalama wa damu, ili kuongeza upatikanaji wa damu salama.

Pia alitoa wito kwa makampuni ya ndani na ya umma pamoja na watu binafsi kuchangia damu kwa wahitaji, ili kuokoa maisha na Kuboresha uchumi wa nchi.

Abdallah Goboka, mmoja wa wakazi wa Chama- Buguruni ambaye ni mmoja ya washiriki katika uchangiaji damu, alizipongeza taasisi hizo kwa jinsi zilivyoendesha zoezi hilo kwa kutoa elimu iliyomuongezea sababu zaidi za kuchangia damu.

# UNESCO yaja na mkakati mwarobaini kukabili maafa

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) linaendesha mafunzo ya wiki mbili kwa wataalamu wa mambo ya maafa kuhusu matumizi ya akili bandia (AI) katika kukusanya takwimu, ili kuyakabili kwa wakati yanapotokea.

Mratibu wa mafunzo hayo kutoka UNESCO, Keven Robert, alisema jana mjini Bagamoyo, kuwa mafunzo hayo yanayotoa uelewa juu ya kukabiliana na maafa yanayosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Pia alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mradi unaoendeshwa katika nchi tano za Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini na Uganda.

Alisema zaidi ya wataalamu 150 nchini wanatarajiwa kufaidika na mafunzo hayo wakiwamo maofisa kutoka jukwaa la maafa nchini, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo huratibu masuala ya maafa, asasi mbalimbali za kiraia na vyuo vya elimu ya juu.

"Kuendeshwa kwa mafunzo hayo kumelenga kuleta teknolojia mpya ya kisasa ya kukabiliana na majanga ikiwa ni pamoja na matumizi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) katika kurekodi taarifa za asili na za sasa za maafa yanayosababishwa na majanga na maeneo ambayo yana majanga au yako katika hatari ya kuwa nayo," alisema.

Mratibu huyo aliongeza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya mradi unaotekelezwa na UNESCO kwa kushirikiana na nchi wanachama kwa ufadhili wa serikali ya Japan.

Pia alisema mradi huo umelenga kuwezesha nchi zisizokuwa na utaratibu maalumu kuwa na sera na sheria zinazohusu majanga na kutoa nafasi kwa walio nazo kuzirejea kwa lengo la kuingiza maarifa ya kisasa katika ukusanyaji wa takwimu na kukabili majanga.

Aidha kwa sasa pamoja na matumizi ya akili bandia, takwimu za majanga hukusanywa na mifumo ya tehama pamoja na kutumia ndege zisizo na rubani kupiga picha zenye maelekezo yaliyokamilika kama eneo la maafa, idadi ya wahusika na athari zake.

"Ni kweli kuwa zaidi ya asilimia 70 ya majanga yanayotokea yanatokana na mabadiliko ya tabia nchi, hivyo mafunzo hayo yameunganisha watu wengi zaidi wakiwamo wanaoshughulika na hali ya hewa," alisema.

Ofisa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa, Charles Msangi, alisema mafunzo hayo yatakuwa na manufaa makubwa sambamba na kuhakikisha wadau wote wanajua namna ya kutumia akili bandia katika shughuli za uokozi. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inashughulikia maafa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 7 ya mwaka 2015 na sera ya taifa ya menejimenti ya maafa ya mwaka 2004.

Alisema ni muhimu kwa wadau wote kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu matumizi ya teknolojia ya akili bandia katika ukusanyaji wa takwimu zinazoweza kuchambuliwa hata kubashiri maeneo, ambayo yanaweza kupata maafa na kuchukua hatua mapema au kuwa tayari.



Mkuu wa Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa (wapili kushoto) na Meneja Mkuu wa NAS Dar Airco Tanzania, Miguel Serra (wapili kulia) walionyesha hati za makubaliano ya kushirikiana katika utoaji wa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa kozi ya anga, 'logistic' na usafirishaji mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT, Nas Dar Airco kushirikiana mafunzo ya anga

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji kimetia saini mkataba wa ushirikiano na Kampuni ya NAS Dar Airco Tanzania katika mipango chanya, ambayo itawasaidia wanafunzi wa mafunzo ya anga na lojistiki katika usafirishaji kupata mafunzo kwa njia ya vitendo.

NAS ilianza shughuli zake Kuwait mwaka 2003 na kuingia Tanzania mwaka 2016, na imebobea katika utoaji wa huduma mbalimbali kwenye zaidi ya viwanja vya ndege 50 ulimwenguni.

Mkataba wa makubaliano ulisainiwa mwishoni wa wiki katika Kampasi ya NIT Mabibo, jijini Dar es Salaam, kati ya Mkuu wa Chuo, Prof. Zacharia Mganilwa na Meneja Mkuu wa NAS Dar Airco Tanzania, Miguel Serra mbele ya mjumbe wa bodi ya NAS Afrika, Prof. Costa Mahalu.

Prof Mahalu alisema kuwa, makubaliano hayo yanakusudia kuanzisha ushirikiano kati ya NAS Tanzania na NIT katika kusaidia wanafunzi kupata mafunzo kwa vitendo.

Prof. Mahalu amlingeza: "Programu ambazo zinatolewa na NIT zinakwenda kukifanya chuo kuwa taasisi bora katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na barani Afrika kwa ujumla."

"Kwa hiyo, NAS Tanzania katika makubaliano haya itatoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya anga na lojistiki na usafirishaji kwa kuhakikisha kuwa wanapata mafunzo bora, ambayo yatasaidia kufanya kazi nje ya nchi," alisema. Kwa upande wake, Prof. Mganilwa alisema makubaliano hayo yatatoa fursa kwa wanafunzi ambao wanasoma kozi za anga, lojistiki na usafirishaji kupata nafasi ya mafunzo kwa vitendo.

Prof. Mganilwa aliongeza kuwa, ushirikiano huo utaboresha na kuiimarisha Shule Kuu ya Usafiri wa Anga na Teknolojia ya NIT kutoa wataalamu zaidi, ambao watasaidia nchi katika sekta ya anga.

Makubaliano hayo yataimarisha mafunzo ya usafiri wa anga, lojistiki na usafirishaji chuoni hapo ambapo hivi karibuni taasisi hiyo ilipata dola za kimarekani milioni 21.25 kutoka Benki ya Dunia, ikilenga kuboresha mafunzo ya anga.

Alisema kupitia Shule Kuu ya Teknolojia ya Usafiri wa Anga iliyopo chuoni hapo imeanza kutoa mafunzo ya usafiri wa anga ya ubobezi, ambapo mpango ni kuzalisha wataalamu wengi, ambao watasaidia uendeshaji katika sekta ya anga nchini.

Meneja Mkuu wa NAS Dar Airco Tanzania alisema NAS Tanzania inafurahi kuingia katika makubaliano hayo na NIT, ili kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi.

Alisema wanafunzi wa NIT watapata uzoefu wa kimataifa na wakati huo huo kupata nafasi za ajira katika ofisi zao, zilizopo katika nchi zaidi ya 20 duniani.

## Mbio Mwenge zilivyoongeza chachu miradi

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema ukimbizaji Mwenge mkoani humo, umeleta mafanikio makubwa ikiwamo kuongeza chachu katika miradi ya kimaendeleo na kuzindua iliyokamilika.

Mwenge huo ulikabidhiwa mkoani humo Agosti 18, ukitokea Mkoa wa Pwani kwa kuzunguka katika wilaya tano zilizopo Dar es Salaam na kuhitimisha mbio zake Agosti 22, mwaka huu wilayani Kigamboni.


Makala aliyasema hayo jana wakati akikabidhi Mwenge huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Terack, baada ya kukamilisha suala la uzinduzi na uwekaji mawe ya msingi katika miradi 46 iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 105.

"Licha ya mafanikio hayo miradi mitano kati ya 46 haikuwezekana kupitishwa na viongozi wa mbio za Mwenge kutokana na kughubikwa na changamoto mbalimbali, ambazo vimesababisha miradi hiyo kutofikia viwango vilivyo tarajiwa," alisema.

Alisema kutokana na changamoto hizo atahakikisha kunakuwa na ufuatiliaji wa kina katika miradi hiyo, ili kutambua dosari zote zilizojitokeza na kukwamisha maendeleo katika maeneo ya uwekezaji na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Wilayani Ilala, Mwenge huo ulipitia miradi ya ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilometa 7.5, stendi ya Kinyerezi na daraja la Ulongoni B, yenye thamani ya Sh. bilioni 17.6, ambalo likikamilika linatarajiwa kuondoa adha ya mafuriko katika maeneo hayo.

Mingine ni ujenzi wa kituo cha polisi Mwanagati, ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji, ujenzi wa madarasa 20 Shule ya Sekondari Kasulu na ujenzi hospitali na kituo cha mfumo wa mapato cha jiji.



Ukurasa 12

**KUELEKEA UCHAGUZI MKUU KENYA**

Uhuru amwambia Naibu Ruto 'out'



Ukurasa 13

**BASIL MRAMBA**

Askari wa mwavuli wa awamu ya tatu



Ukurasa 14

**Hakainde Hichilema atinga Ikulu**

siasa

JUMATANO AGOSTI 25, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Mapendekezo wadau NEC yanapoibua mjadala zaidi

## • Ni matamanio ya uchaguzi na haki

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuiagiza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kupitia sheria za uchaguzi na kushirikisha wadau kwenye mchakato wa mapendekezo hayo, wachambuzi wa siasa wanasema suluhu ni katiba mpya itakayoleta tume huru ya uchaguzi.

Mjumbe wa Baraza Kuu la CUF, Taifa, Abdul Kambaya, anasema pamoja na Rais kuruhusu mjadala na mapendekezo ya wadau, suluhisho la yote ni kuwa na katiba na tume huru.

Rais Samia alitoa maagizo hayo, hivi karibuni, wakati akipokea taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, 2020 iliyowasilishwa kwake na NEC

Kambaya akirejea maelekezo hayo anasema: "Uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, dunia iliahidiwa kwamba utakuwa huru na haki. Lakini tunajua kilichotokea, hivyo hata suala hili linaweza kutatuliwa na tume huru inayotokana na katiba mpya."

Anaeleza kuwa tume huru inayotokana na katiba mpya, ni mwiba wa kasoro zote, kwa kuwa haitaegemea upande wowote, na kwamba itaondoa malalamiko yanayojitokeza kila uchaguzi.

"Kumbuka hata uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019, Watanzania waliahidiwa kwamba utakuwa huru, lakini figisu zilikuwa nyingi kuanzia wagombea kuchukua fomu hadi kuzirejesha," anakumbusha Kambaya.

Wasimamizi walifunga ofisi na kusababisha wagombea wa upinzani kukwama kuwasilisha fomu kwa wakati au kukosa fomu za kuomba kuwania nafasi za uongozi wa serikali za mitaa, anaongeza.

"Uwepo wa tume huru ya uchaguzi ndiyo suluhisho la yote hayo, kwani pamoja na ahadi za serikali kuruhusu mjadala wa mapendekezo ya wadau, hata wakurugenzi wa halmashauri wakiondolewa katika usimamizi wa uchaguzi, bado tume iliyopo viongozi wake wanateuliwa na Ikulu, hivyo tatizo liko pale pale," anasisitiza.

Anasema uzoefu unaonyesha kuwa imekuwa ni kawaida kuvuruga uchaguzi kwa madai ya kulinda maslahi ya wachache na kuzusha malalamiko ambayo kama kungekuwa na tume huru yasingekuwapo.

Wakati ikiwasilisha mapendekezo ya wadau kuboresha uchaguzi mkuu wa 2025, inataja uwezekano wa kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura 292 kuwa ni miongoni mwa yaliyopendekezwa.

Aidha, mengine ni kutaka uchaguzi wa serikali za mitaa kusimamiwa na mamlaka moja.

Pamoja na hayo, mapendekezo mengine ni umuhimu wa NEC kuwa na wafanyakazi wenye ngazi ya halmashauri badala ya kuwatumia wakurugenzi wa halmashauri.

Aidha, ilipendekezwa serikali kutoa fedha kwa ajili ya asasi za kiraia zinazotoa elimu ya mpigakura.

Rais Samia, anakumbusha kuwa katika uchaguzi huo, yapo matatizo yaliyojitokeza na ndiyo moja ya sababu ya kuandaliwa kwa ripoti hiyo na kuwekwa hadharani ili kutoa fursa kwa wadau wa uchaguzi na wananchi kuichambua na kutoa mapendekezo yao.

Anasema, jambo la muhimu ni wadau kujadili kwa kina, kwa kuwa kila suala linaloanzishwa lina msingi wake, kwamba, ili uchaguzi ukidhi malengo, ni lazima usimamiwe kikamilifu , lakini kinyume chake unaweza ukawa chanzo cha fujo na vurugu kama ambavyo imekuwa ikishuhudiwa katika baadhi ya nchi..

Anabainisha kuwa, mapendekezo yaliyotolewa na wadau ni ya msingi, na kwamba cha umuhimu ni kuyajadili kwa kina.

Maelekezo ya Rais Samia, yanafanana na yale yaliyowahi kutolewa baada ya mchakato wa katiba mpya kukwama 2014, ya kuelekeza baadhi ya sheria za uchaguzi kuangaliwa upya ili kuufanya uwe huru, haki na unaokubalika.

Baadhi ya mapendekezo hayo ni kuangalia kuwapo kwa tume huru inayosimamia uchaguzi huo, aidha kuzitazama upya asilimia za ushindi kuwa mshindi apate zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa, lakini pia kuruhusu matokeo ya urais kupinga mahakamani na kuwapa nafasi wagombea huru.



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji mstaafu Semestocles Kaijage (kulia), akisoma taarifa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, katika hafla ya kukabidhi Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. **PICHA: MTANDAO**

**NI MWANZO MZURI**

Wakiendelea kutoa maoni yao, baadhi ya wachambuzi wanaeleza kile wanachokitarajia na kwamba ni mwanzo mzuri.


Mchambuzi wa siasa Maggid Mjengwa, anasema, kuwapo kwa mapendekezo ya wadau na pia maoni ya Rais kuruhusu mjadala wa mabadiliko kwenye sheria za uchaguzi ni mwanzo mzuri kwa kuwa inaonyesha ni jinsi gani Rais alivyo tayari kufanya mabadiliko kwa manufaa ya Watanzania wote bila kujali maslahi ya vyama.

**INAENDELEA UK.14**

# Kuelekea uchaguzi mkuu Kenya 2022

## • Uhuru amwambia Naibu Ruto 'out'

Na Mwandishi Wetu



Watetezi wa mkakati wa BBI, Rais Uhuru Kenyata (kulia) na Raila Odinga, wamepingwa na Mahakama ya Rufani kuhusu kubadili katiba ili kuweka mapendekezo ya mkakati huo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

BAADA ya Mahakama ya Rufani nchini Kenya kutupilia mbali mchakato wa mabadiliko ya katiba uliopendekezwa na BBI, ulioasisiwa na Rais Uhuru Kenyatta na mwanasiasa wa upinzani Raila Odinga, Kenyata ameanza kumfukuza naibu wake.

Amemtaka Naibu William Ruto, aondoke serikalini badala ya kuendelea kuishambulia akiwa yuko ndani yake.

Uamuzi huo wa mahakama wa kukataa kubadili katiba ili kuingiza mapendekezo ya Kenyata na Raila ni furaha kwa Ruto, ambaye tangu mwanzo alikuwa akipinga BBI

Kwa mujibu wa BBC, uamuzi huo unaonekana ushindi kwa wanasiasa waliokuwa wanapinga mchakato huo, wakiongozwa na Naibu Rais Ruto ambaye ametangaza nia ya kugombea urais mwakani kwenye uchaguzi utakaofanyika Agosti 9, 2022, kupitia chama cha United Democratic Alliance (UDA).

BBC inasema iwapo hakutakuwa na rufaa nyingine kwenda kwenye Mahakama ya Juu, ratiba ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu Agosti 9 mwaka 2022 itabakia kama ilivyo kwa sababu hakutakuwa na kura ya uamuzi.

### MCHAKATO WA BBI

Mchakato wa kutaka kuibadilisha katiba ya nchi hiyo iliyopatikana mwaka 2010, ulianza baada ya Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, kumaliza uhasama wao kisiasa na kuungana ili kubadilisha mfumo wa uongozi nchini humo, kwa kuanzisha kile walichokiita 'Building Bridges Initiative' -BBI.

Siku tano baada ya kutolewa hukumu hiyo, Rais Uhuru anamtaka Naibu Ruto, aondoke serikalini badala ya kushambulia serikali ambayo yuko ndani yake.

Naibu amefurahishwa na uamuzi wa mahakama hiyo, kwa sababu tangu mwanzo, Ruto alivurugwa na BBI, mkakati wa Kenyata na Odinga wa kujenga Kenya mpya uliokuja na mapendekezo ya kubadilisha katiba ili kuunganisha kiungozi makabila ya nchi hiyo na kuleta umoja.

Ruto na washirika wake waliamini kuwa kumleta hasimu wao Odinga kwenye meza ya pamoja kupitia mkakati wa BBI ni mpango wa kugawana madaraka baina yake na Kenyata ambaye waliona atamuunga mkono Odinga kwenye kugombea urais na kumtosa Ruto wakati wa uchaguzi mkuu wa Agosti 2022.

### KUFUKUZWA SERIKALINI

Jumatatu wiki hii Kenyata amewasha moto jijini Nairobi, akiwaambia wahariri nchini humo kuwa amekasirishwa na ukosoaji uliotolewa dhidi ya utawala wake na kambi ya Ruto.

Rais huyo anasema hakuwa na ufahamu wowote kwa nini upande wa Naibu Ruto umechagua mashambulio dhidi ya utawala wake.

Anawaambia waandishi wa habari kwamba hana shida na Ruto kujenga ngome yake kisiasa lakini alihoji mbinu anazotumia akitumia chama kipya alichokiunda cha United Democratic Alliance (UDA).



Naibu Rais, William Ruto.

> Ikiwa ninataka sasa kuboresha zaidi kuna tatizo gani? Tukirudi nyuma hadi mwaka wa 2013 imekuwa ajenda yangu ya kuleta watu pamoja.

"Sijui nini kimetokea isipokuwa ukweli ni kwamba anajaribu kujenga ngome yake ya kisiasa. Ninahisi ni bahati mbaya jinsi anavyofanya... ni vibaya," anasema.

Uhuru anaongeza kuwa anashangaa kwanini naibu wake alikuwa akipinga mchakato wa BBI akisema "masuala yaliyopelekea kuundwa kwa BBI ndiyo yaleyale yaliyowaleta pamoja".

"Ikiwa ninataka sasa kuboresha zaidi kuna tatizo gani? Tukirudi nyuma hadi mwaka wa 2013 imekuwa ajenda yangu ya kuleta watu pamoja," anasema.

"Ikiwa mgawanyiko wa 2007 ulituleta pamoja, kuna shida tukiwaleta watu wengine ndani?" anahoji

Rais huyo anasema hatua yake ya kuiunganisha nchi hiyo haimaanishi kupunguza nafasi za mtu yeyote kumrithi.

"Haikunyimi nafasi zako siyo Uhuru anayechagua, ni Wakenya wanaopiga kura."

Anawaambia wahiriri kuwa masuala kadhaa yaliyosababisha mgawanyiko unaotikisa utawala wake yanatokana na ari yake ya kuleta umoja.

### HANA LA KUFANYA

Licha ya mchakato wa kurekebisha katiba unaotokana na BBI kuleta mgawanyiko kati ya Rais Kenyatta na Naibu Ruto ambao walishinda uchaguzi mara mbili wakigombea kwa tiketi moja ya Jubilee, Kenyatta hana la kufanya.

Kwa mujibu wa katiba Rais hawezi kumfukuza Naibu wake, hatua hiyo ndiyo inayosababisha amtake Ruto kuondoka serikalini. Licha ya kuendelea na kampeni zake za urais mwakani, Ruto amekuwa akieleza mafanikio ya serikali ya Jubilee huku wakati mwingine akikosoa baadhi ya sera na uamuzi unaofanywa na serikali.

Miongoni mwa mambo hayo ni mchakato wa BBI na ushirikiano wa karibu wa Rais Kenyatta na viongozi wa upinzani hasa kiongozi wa ODM Raila Odinga.

Hata hivyo kambi ya Ruto au chama cha UDA hakijasema lolote kuhusu tamko hilo la Rais la kumtaka aondoke serikalini .

### NITAONDOKA NIKITAKA

Kwa mujibu wa gazeti la the Standard la Kenya, mwanzoni mwa mwezi huu, Naibu Rais William Rutto, alitangaza kuwa ataondoka serikali kwa wakati atakapoamua.

Baada ya Ruto kuunda UDA, anawaambia washirika wake kuwa wamepata makazi mapya, wana vitu vyao ikiwamo bendera zao na kwamba makazi ya zamani ya Muungano wa Jubilee, yamebomoka.

"Sisi siyo wageni wa mambo haya. Tunachagua kujiunga na vyama kwa hiari yetu, kadhalika tunaamua kuondoka tukiona inafaa. Hakuna wa kutuuliza mbona bado tunaendelea kubaki si kazi yake," anasema Ruto, anapoulizwa kwani haondoki anaendelea kuwa king'ang'azi kwenye serikali anayoamini kuwa imefeli kutimiza ahadi za uchaguzi.

Ruto anamtuhumu Rais Uhuru Kenyatta kwa kushirikiana na kambi ya ODM ya Raila Odinga na kutembelea ajenda zao na sasa serikali yake imeshindwa na haina cha kujivunia.

### HISTORIA YA MAFARAKANO

Pamoja na BBI, iliyoonekana kumtenga Ruto na kumkumbatia Odinga, tatizo lilikolea zaidi mwaka 2019 baada ya Uhuru na Kenyatta kuonekana kuwa hawaivi kufuatia hatua ya kukamatwa kwa Waziri wa Fedha Henry Rotich, kwa tuhuma za ufisadi.

Rotich, alijisalimisha kwa maofisa wa upelelezi Julai 2019 baada kutuhumiwa kulipa zaidi ya dola milioni 450 kugharamia ujenzi wa mabwawa mawili nchini humo kwa kampuni ya Italia.

Anatuhumiwa kukiuka mwongozo wa utoaji wa kandarasi iliyoopewa kampuni ya Italia CMC de Ravenna yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 450 kwa ujenzi wa mabwawa hayo, hatua ilimchukiza Ruto.

Rotich, ni mshirika mkubwa wa Ruto , eneo la Kaskazini la Rift Valley na aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha kwa mapendekezo ya Ruto kwa Kenyatta.

Mgawanyiko ndani ya Jubilee, ulikolezwa na kampeni ya Kenyata ya kupambana na ufisadi uliowatia kashkash Rotich na maofisa wenzake 20 wa hazina kwa madai ya upotevu wa bilioni 21 (Dola milioni 203) kwenye ujenzi wa mabwawa hewa ya Arror na Kimwarer.

BASIL MRAMBA

# Askari wa mwavuli wa awamu ya tatu

Na Mary Geofrey

• Mwasisi SIDO, mnunuzi ndege ya Rais Mkapa



Basil Mramba (kulia), Daniel Yona na Gray Mgonja (kushoto), wakati wa kesi ya matumizi mabaya ya madaraka, **PICHA: MTANDAO**

WAZIRI aliyelitumikia taifa kwa muda mrefu akihusika na kuanzisha mashirika, kuongoza wizara na hata kufuta baadhi ya kodi umiza, licha ya kutwaliwa kwenye maisha ya utukufu, ataendelea kukumbukwa.

Ni Basil Mramba, aliyekuwa Waziri wa Fedha kwenye awamu ya kwanza na ya tatu ya Benjamin Mkapa. Mramba alifariki dunia Jumanne Agosti 17, akiwa na miaka 81, baada ya kuitumikia nchi kwa wadhifa wa Waziri wa Fedha, Viwanda na Biashara, mbunge lakini pia mkurugenzi na mwasisi wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO).

Waziri huyo atakumbukwa kwa mengi lakini eneo mojawapo ni kuwaondolea Watanzania kero ya kodi sumbufu ya maendeleo, baiskeli na mifugo. Yote hayo yalifanyika katika awamu ya tatu.

Mramba aliyezaliwa mwaka 1940, ni msomi, aliyehitimu katika Chuo Kikuu cha Makerere Uganda na kupata shahada ya kwanza na baadaye aliendelea na masomo katika Chuo Kikuu cha City jijini London, Uingereza na kupata shahada ya uzamili katika biashara.

Baada ya kurejea nchini, Mramba alifanya kazi serikalini katika nyadhifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa mwanasiasa na mbunge wa jimbo la Rombo.

Aidha, aliwahi kuwa Waziri wa Fedha katika awamu ya tatu kuanzia 2001 hadi 2005. Lakini pia aliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuanzia 1995 hadi 2000.

Jambo jingine litakalomfanya Mramba akumbukwe ni kuanzisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na yeye akiwa mkurugenzi wake wa kwanza. Shirika hilo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 28 ya mwaka 1973 na Mramba anaelezwa kuwa aliliongoza kwa ufanisi mkubwa.

Rais Mkapa alimteua kuwa Waziri wa Fedha na kutekeleza majukumu yake kipindi ambacho nchi ilikuwa ikifanya maboresho kwenye taasisi nyingi za umma kuanzia za fedha, uongozi, mahakama, elimu pamoja na kuanzisha nyingine mpya ikiwamo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Uteuzi wa Mramba haukuwa mpya kwenye safu ya uongozi kwa vile aliwahi kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara wakati wa awamu zilizotangulia.

### ATAKAVYOKUMBUKWA

Mramba atakumbukwa kwa kuendelea kuzishawishi taasisi za fedha za kimataifa, kuisamehe Tanzania madeni makubwa yaliyokuwa ni mzigo kwa serikali na kufanikiwa kupunguza deni la taifa kwa karibu asilimia 50.

Mwaka 1996 Benki ya Dunia (WB) pamoja na Shirika la Fedha Duniani (IMF) zikihusisha taasisi nyingine za fedha ikiwa nchi au taasisi kwa pamoja (multilateral) au kwa pamoja (bilateral) zilianzisha utaratibu wa kuzungumza na na kuzisaidia nchi maskini na zenye madeni makubwa zisiumizwe na mzigo wa madeni na kuanzisha utaratibu wa kuzipunguzia mizigo hiyo na kuzipa mikopo na misaada yenye unafuu baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa.

### KUBINAFSISHA MASHIRIKA

Mramba ni miongoni mwa viongozi wakuu ambao walisimamia ubinafsishaji wa mashirika ya umma, ambayo kimsingi ni mali ya serikali yakisimamiwa na Msajili wa Hazina.

Wakati Mramba akiwa Waziri wa Fedha, masuala yaliyohusu ubinafsishaji yalikuwa yakieleza kuwa takribani mashirika ya umma 2,000 yalikuwa na hali mbaya kiuchumi, kifedha na kiuongozi hivyo yalihitaji mabadiliko na ikiwezekana yaondolewe kwenye mikono ya serikali na kukabidhiwa wawekezaji binafsi kwa ajili ya kuyaendesha kwa tija ili yachangie kodi serikalini badala ya kuitegemea kwa ruzuku.

Baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa wakati wa uongozi wa Mramba ni pamoja na Kitengo cha Makontena cha Mamlaka ya Bandari (THA) kutenganisha Shirika la Posta na Simu na kuunda Kampuni ya Simu TTCL na Shirika la Posta, kubinafsisha Mamlaka ya Maji Dar (DAWASA) na Shirika la Ndege la Taifa (ATC).

Pamoja na juhudi hizo Mramba atakumbukwa kwa kusimamia uanzishwaji wa sekta binafsi na serikali kuiunga mkono ili ikue na kuwa injini ya uchumi.

### UNUNUZI WA NDEGE

Mramba atakumbukwa kwa msimamo wake katika ununuzi wa ndege ya Rais ulioibua mjadala kwa baadhi ya wananchi na wanasiasa hasa wa kambi ya upinzani.

Wakati huo akiwa Waziri wa Fedha, Mramba alisimama imara na kutetea ununuzi wa ndege ya Rais kwa ajili ya safari za mkuu wa nchi na kusisitiza kuwa Watanzania wako tayari kula majani ili kiongozi wao apate ndege.

Katika kutetea hoja ya ununuzi wa ndege ya Rais, Mramba alitoa kauli akisema: "Watanzania tuko tayari kula nyasi ilimradi ndege ya Rais inunuliwe," msimamo huo uliwakera baadhi ya watu, ilisisitiza umuhimu wa nchi kuwa na ndege ya Rais na hakurudi nyuma hadi ilipopatikana.

Kauli hiyo ya Mramba iliendelea kudumu na kuzunguka katika kumbukumbu za watu hata alipostaafu katika utumishi wake mwaka 2005.

### KUFUNGULIWA MASHTAKA

Mramba, Daniel Yona na Gray Mgonja, walishitakiwa kwa matumizi mabaya ya ofisi, ikidaiwa kuwa kati ya Agosti 2002 na Juni 14, 2004 jijini Dar es Salaam waliisamehe kodi kampuni ya Ukaguzi wa Madini ya Alex Stewart Government Business Assayers ya Uingereza kinyume cha sheria na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 11.7.

Julai 7, 2015, Mramba na Yona aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, walihukumiwa kila mmoja kifungo cha miaka mitatu jela na kulipa faini ya Sh. milioni 5 baada ya kupatikana na hatia ya matumizi mabaya ya madaraka.

Mramba, Yona pamoja na aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Grey Mgonja, wote kwa pamoja walikuwa wakikabiliwa na jumla ya mashtaka 11 ya kutumia madaraka yao vibaya na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 11.7.

> Februari 6, 2016, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliamuru wafungwa hao wabadilishiwe kifungo kutoka gerezani na kufanyakazi za jamii.

Walidaiwa kuwa katika utumishi wao wa umma walitumia vibaya madaraka yao kwa nafasi zao na kuisababishia serikali hasara ya kiasi hicho cha fedha.

Kesi hiyo ilikuwa ikisikilizwa na Jaji John Utamwa, Jaji Sam Rumanyika na Saul Kinemela, lakini wakati wa hukumu jopo hilo lilitofautiana na hivyo kuwa na hukumu mbili.

Hukumu ya kwanza ilikuwa ya wengi (wawili) ambayo iliwatia hatiani Mramba na Yona na kumwachia huru Mgonja, iliyosomwa na Jaji Rumanyika na hukumu ya wachache (mmoja) ambayo hata hivyo, haikusomwa siku hiyo.

Wawili hao walikata rufaa Mahakama Kuu, kupinga adhabu, lakini wakati wakikata rufaa, serikali pia kwa upande wake ilikata rufaa dhidi yao ikipinga adhabu waliyoepewa ya kulipa fidia ya Sh. milioni tano, badala ya kulipa hasara yote waliyoisababisha. Serikali ilikata rufaa dhidi ya Mgonja ikipinga hukumu ya Mahakama ya Kisutu kumwachia huru.

### ADHABU YABADILIKA

Februari 6, 2016, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliamuru wafungwa hao wabadilishiwe kifungo kutoka gerezani na kufanyakazi za jamii.

Walitumikia kifungo cha nje kumalizia sehemu ya adhabu yao ya miaka miwili iliyobakia kwa kufanya huduma za kijamii, kusafisha hospitali ya Sinza Palestina kwa saa nne kila siku kwa siku tano za kazi hadi walipomaliza kifungo Novemba 5, 2016.

# Hakainde Hichilema atinga Ikulu

## • Mtihani mkubwa unaomngoja, ukosefu ajira, fedha mfukoni

**Na Salome Kitomari**

RAIS Hakainde Hichilema (59), ameapa kuwatumikia Wazambia jana, baada ya kuibuka mshindi dhidi ya mpinzani wake Edgar Lungu. Wakati anaingia ikulu, matarajio ya waliompigia kura ni makubwa hasa kumaliza ukata mkubwa unaowakabili na ukosefu wa ajira ambao ulipelekea baadhi ya wapigakura kwenda kwenye vituo vya kura wakiwa wamevalia majoho ya kuhitimu elimu ya juu lakini hawajapata kazi.

Hichilema kiongozi wa chama cha United Party for National Development (UPND), ana sifa nyingi ikiwamo ujasiri kwani alijaribu kugombea mara tano bila mafanikio, ni mhanga wa kesi za uhaini, alikamtwa na kuwekwa ndani wakati wa kampeni, amevamiwa na kufanyiwa vurugu wakati wa mahojiano na chombo cha habari.

Akiwa na wenzake 14 walinyimwa kufanya kampeni kwa kisingizio cha kuwapo corona inayozuia mikusanyiko, huku chama tawala cha Patriotic Front (PF) kikiendeleza kazi majukwaani, kuwazuia kulilenga kudhibiti ushindani mkubwa ulikuwapo kati yake na rais aliyeshindwa.

Kwa sasa matarajio ya wananchi wa Zambia ni mabadiliko ya kiuchumi kwa kuwa na mzunguko wa fedha, ukuaji wa sekta binafsi, ongezeko la ajira na uhuru wa maoni na wa vyombo vya habari.

Aidha, Rais huyo, ameamsha furaha baada ya kuahidi kutolipa kisasi kwa watesi wake, kuahidi uhuru wa vyombo vya habari kufanyakazi yake kwa mujibu wa sheria na kuacha upendeleo kama ilivyofanyika wakati wa uongozi wa Lungu.

Takwimu za nchi hiyo zinaonyesha ukuaji wa uchumi unabadilika kila mwaka, wakati 2018 ulikuwa asilimia nne, 2019 ulishuka hadi 1.5, na kupanda hadi asilimia 2.3 mwaka 2020.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia mwaka 2020, uwapo wa corona ulishusha thamani ya Kwacha fedha ya Zambia kwa asilimia 30, kuongeza madeni ya nje huku taasisi za fedha zikiwa taabani na mamia kupoteza ajira.



Rais Hakainde Hichilema, maarufu 'HH' amechukua uongozi wa nchi hiyo rasmi baada ya kushinda kwa kishindo. **PICHA: MTANDAO**

> Akiwa na wenzake 14 walinyimwa kufanya kampeni kwa kisingizio cha kuwapo corona...

### HALI ILIVYOKUWA

Siku ya kupiga kura mitandao ilipunguzwa nguvu na wengi kushindwa kutumia mitandao ya kijamii, kutuma na kupokea picha na video mbalimbali, jambo ambalo lilipingwa vikali na wananchi na baadaye Mahakama Kuu, iliamuru serikali kuifungua

Aidha, Rais Lungua usiku wa kupiga kura alitoa taarifa kwa vyombo vya habari akimshutumu Hichilema na wafuasi wake kwa kufanya vurugu kwenye jimbo la Mashariki Magharibi mwa nchi hiyo na kusababisha vifo vya maofisa wawili wa chama cha PF na kuahidi kuchukua hatua .

Aidha, siku iliyofuata alitangaza kutoridhishwa na mchakato wa uchaguzi kwa kile alichodai kuwepo kwa rafu nyingi, lakini baada ya matokeo kutangazwa usiku wa Agosti 13, mwaka huu na Tume ya Uchaguzi Zambia, alikubali kushindwa.

Kwa mujibu wa tume hiyo, watu 1,023,499 walijiandikisha kwenye daftari la wapiga kura wengi wakiwa ni wanawake na kundi kubwa ni vijana wenye umri usiozidi miaka 35 ambao walimchagua rais, wabunge 156 , diwani na meya na baada ya serikali kuingia madarakani rais ana nafasi 10 za kuteua na kufanya jumla ya wabunge 166.

Matokeo yaliyotangazwa na chama tawala , PF kilipata majimbo 72 wakati UPND ya Hichilema ikizoa majimbo 83 naye akishinda kwa zaidi ya kura milioni 2.8 , wakati Lungu akiambulia milioni 1.8 kukiwa na tofauti ya kura zaidi ya 1000,000.

Ikilinganishwa na uchaguzi wa nchi nyingi za Afrika, Zambia wananchi wanachagua meya wa serikali za mitaa, lakini pia wafungwa waliwekewa vituo vya kupiga kura na walipata nafasi ya kutimiza wajibu wa kikatiba.

### KILICHOMWANGUSHA LUNGU

Wachambuzi wa siasa nchini humo, wanaokutana na waangalizi wa uchaguzi wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA), wanaeleza kuwa makada wa PF walikuwa wakifanya vurugu kwenye vyombo vya habari na takribani radio saba zilivamiwa na vifaa kuharibiwa, huku waandishi wakipigwa.

Aidha, hali ngumu ya maisha hasa kukosekana fedha na ajira ni sababu kubwa ya wananchi kutaka mabadiliko. Kadhalika kukithiri ufisadi serikalini nako kulichangia. Utafiti uliofanywa Julai 2020 na Chuo Kikuu cha Gothenburg's kwenye serikali kuu na za mitaa ulibaini viongozi walitumia ujio wa corona kujipatia madaraka na kujitajirisha.

Aidha, dola za Marekani milioni 4.3 zilizotolewa na Sweden na Ireland kusaidia watu maskini nchini humo zilipotea katika mazingira tatanishi bila kuwafikia walengwa. Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya rushwa (Transparency Internationals' 2019 Corruption Perception Index) Zambia ilikuwa ya 113 kati ya mataifa 180, huku uwezo wa kupambana na rushwa ukizidi kushuka na wananchi wengi kubakia maskini na wachache wakitajirika.

Aidha, serikali ya Lungu ililaumiwa kwa kufungia vyombo vya habari ikiwamo kuwafukuza kazi walokuwa wanafanyakazi kwenye vyombo vya umma kabla ya Lungu kuingia madarakani na pia kubinya uhuru wa wanahabari na kuvipangia cha kuripoti.

***Mwandishi alikuwa mwangalizi wa uchaguzi mkuu wa Zambia.***

# Mapendekezo wadau NEC yanapoibua mjadala zaidi

**INATOKA UK.11**

"Kwa mfano mapendekezo ya wadau kwamba NEC iwe na watumishi kwenye ngazi ya halmashauri ni muhimu, kutokana na kwamba kumekuwapo na sintofahamu kila unapofanyika uchaguzi," anasema Mjengwa.

Wakurugenzi wa halmashauri wanalaumiwa kwa kuwaengua baadhi ya wagombea kwenye uchaguzi hata kwa jambo dogo ambalo wangetumia busara kulimaliza.

" Rais ametolea mfano masuala ya kiufundi, kama kukosea kuandika jina la mgombea au chama na kwamba yasitumike kumnyima haki ya kushiriki uchaguzi," anasema.

Anasema iwapo mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi, imani ya wananchi kwa tume itaongezeka na kupunguza hofu inayotokana na yale ambayo yamekuwa wakidaiwa kufanywa na baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri.

"Hata Tume ya Jaji Warioba kwenye rasimu ya katiba, iligusia suala la NEC kuwa na watumishi ngazi ya chini ili kuondoa kasoro zinazojitokeza kila unapofanyika uchaguzi na nyingine kuhusishwa na hofu ya wasimamizi wakiwaogopa waliowateua," anasema.

### AIBU ZITAPUNGUA

Mwenyekiti wa Taasisi Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anasema, aibu za mara kwa mara kwenye uchaguzi zinaweza kupungua iwapo kuna usimamizi imara.

"Kumekuwapo na mambo ya aibu kwenye uchaguzi ambayo husababishwa na baadhi ya wasimamizi kama kuwanyima mawakala nakala za viapo vya kusimamia uchaguzi au kuwaengua wagombea kwa sababu zinazolalamikiwa na kuonekana hazina mashiko," anasema Ngawaiya.

Anasema, wao kama watu wa utawala bora, wanaamini kwamba, tume huru yenye watumishi ngazi zote itapunguza kasoro zisizo za lazima ambazo baadhi husababishwa na wasimamizi watumishi wa serikali.

### KUONDOKA MAKADA

Ngawaiya anasema, chanzo kikubwa cha kasoro kinatokana na kwamba baadhi ya wasimamizi ni makada wa chama, hivyo inawawia vigumu kuruhusu wagombea wa upinzani kushinda.

"Niseme tu kwamba, figisu kama kukosea kuandika majina yao au vyama vyao, ni aibu na udhaifu wa kutaka ushindi wa mezani badala ya kupambana majukwaani, " anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, si vyema kuwanyuma wapigakura mgombea wanayemtaka kwa lengo la kufurahisha ngazi ya uteuzi, kwa kuwa husababisha kupata viongozi ambao si chaguo lao.





# USAID kusaidia utoaji elimu afya

Na Augusta Njoji, DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo la Marekani (USAID) Tanzania, limeahidi kuendelea kuisaidia serikali katika uanzishaji wa mfumo thabiti ya kusaidia utoaji wa elimu ya afya kwa umma ili kuleta matokeo chanya.

Mkurugenzi wa Afya wa USAID Tanzania, Anathy Thambinayagam aliyasema hayo juzi jijini hapa kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa kuhimiza Afya Tanzania.

Alisema USAID inaiunga mkono Tanzania kupitia mradi wake wa 'Tulonge Afya' kupitia Jukwaa la kidigitali la kukuza Afya (HPDP) ambapo kitovu cha habari kitatumiwa na serikali kusambaza habari za afya kwa umma.

Alisema mfumo uliowekwa wa mawasiliano ya afya utasaidia kudumisha usawa na kukuza utoaji elimu kwa umma.

"Tunayo furaha kuwa sehemu ya msaada huu, ambao umewezesha sehemu ya kukuza afya kufikia hatua zake za sasa, tunatumaini kuendelea kushirikiana kama washirika katika kuboresha maisha ya Watanzania,"alisema.

Hata hivyo, alisema katika kuboresha uratibu wa shughuli za Mabadiliko ya Jamii na Tabia (SBC), USAID Tulonge Afya iliunga mkono kuanzishwa kwa Jumuiya za Utendaji za SBC katika mikoa 12, ambayo inaleta pamoja wadau katika mikoa hiyo na kuhamasisha rasilimali zilizopo kusaidia kuleta mabadiliko kwa jamii.

"Tunajua kuwa kukuza afya na mabadiliko ya kijamii na tabia huchukua jukumu muhimu katika kushughulikia hali ya tabia na kijamii ya kuzuia na kudhibiti magonjwa. Ikifanywa vizuri, mabadiliko ya kijamii na kitabia huipa umma habari sahihi, wazi, inayofaa kwa wakati na husaidia kufanya uamuzi ambao mwisho wake jamii huwa na afya na ustawi zaidi,"alisema.

Kadhalika, alisema hivi sasa dunia inakabiliwa na janga la corona, USAID kupitia mradi wa Tulonge Afya, imesaidia namna ya kukabiliana na vihatarishi katika shughuli jamii ili kukabiliana na janga hilo.

"Tunaunga mkono maendeleo ya mkakati wa mawasiliano ili kuongeza mahitaji ya chanjo za corona, mkakati huu unatarajiwa kuongeza matumizi ya chanjo hizo kwa kutumia njia za SBC zilizo na ushahidi, kutoa habari halisi kwa walengwa, na kushughulikia uvumi wote, imani potofu," alisema.

# Waziri ataka elimu ya corona kijiji kwa kijiji

Na Paul Mabeja, DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, amewataka waganga wakuu wa mikoa kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kupata chanjo ya corona badala ya kukaa ofisini.

Dk. Mollel alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kongamano la umuhimu wa utoaji huduma za elimu ya afya kwa umma.

Alisema kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona wimbi la tatu nchini, wataalamu wa afya wanatakiwa kubadili mbinu za kuukabili kwa kutoa elimu za huduma za afya kwa umma. Naibu Waziri huyo alisema hivi sasa serikali inatoa chanjo kwa wananchi wanaohitaji ili kukabiliana na ugonjwa huo lakini kuna haja kwa wananchi kupewa elimu itakayowasaidia kubadili mitazamo yao.

"Makongamano na semina hivi sasa havina maana bali kinachohitajika ni ninyi wataalamu wa afya kwenda kijiji kwa kijiji kukutana na wananchi kuwaelimisha ili wahamasike na kutambua umuhimu wa wao kuchanja chanjo hii ya kujikinga na UVIKO-19,"alisema.

Aidha, alisema wananchi walioko maeneo ya vijijini bado hawajapata elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa chanjo inayotolewa hivi sasa na serikali.

Alisema ili serikali ifanikiwe katika chanjo, wataalamu wanatakiwa kubadili tabia zao za kujifungia ofisi na kuwaacha wananchi bila maarifa ya kutambua faida au hasara za kutopata chanjo hiyo.

"Ni lazima kama tunataka kufanikiwa jambo hili liwe shirikishi sana. Watu wote tuwe kitu kimoja tutumie hata redio za kijamii katika maeneo ya wananchi ambazo zinatumia kutangaza kwa lugha zao kama vile Kisukuma na Kimasai ili kufikisha ujumbe vilivyo," alisema.

Pia alisema matumizi ya vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii ni muhimu sana kuzipa kipaumbele ili kuwafikia watu wengi na kwa ufanisi mkubwa.

Akiwasilisha mada katika kongamano hilo, Prof. Deodatus Kakoko, kutoka Chuo cha Afya na Sayansi za Jamii Muhimbili, alisema tabia ndiyo kikwazo kikubwa kwenye kukabiliana na corona.

Alisema suala la tabia ndilo limebeba kila kitu katika kufanikisha utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa wananchi.



Mbunge wa Jimbo la Bahi, mkoani Dodoma, Keneth Nolo, akizungumza na wananchi kwenye sherehe ya Maulid, katika viwanja vya Msikiti wa Taqwa Kigwe, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil. 4.5/- zasaidia wenye uhitaji maalum

Na Peter Mkwavila, DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, amesema katika kipindi cha mwaka 2020/21, serikali imenunua na kusambaza katika shule vifaa visaidizi maalum, kwa ajili ya watoto wenye uhitaji maalum vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.5.

Pia amezitaka mamlaka zote zinazohusika katika ngazi za mkoa na halmashauri, kuhakikisha vifaa hivyo vimewafikia wanafunzi walengwa na vinatumika kama vilivyokusudiwa kwa mustakabali wa elimu ya wanafunzi wenye uhitaji maalum.

Silinde aliyasema hayo alipokuwa akizungumza kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa Umoja wa Maofisa Elimu Maalum Tanzania Bara (UMEMTA) uliofanyika jijini hapa.

Alisema kutokana na msaada huo, serikali inaendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ndogo ya elimu maalum na kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya madarasa, vyoo, mabweni, ununuzi wa vifaa na visaidizi maalum pamoja na uboreshaji wa mazingira ya shule pamoja na kuajiri walimu wataalamu kila inapopata fedha.

Pia alisema serikali inaendelea kuhimiza utoaji wa elimu jumuishi kwa kuzingatia mkakati wa kitaifa, ili kuondoa ubaguzi, unyanyapaa na kutengwa kwa watoto ndani ya jamii, hivyo maofisa hao wanakuwa wataalamu wa eneo hilo na watawajibika katika kutoa uelewa kwa jamii kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

"Natambua kuwa majukumu yenu ya msingi katika eneo la elimu maalum ni kusimamia utoji wa elimu kwa wanafunzi wenye uhitaji maalumu ambao wamegawanyika katika makundi ya wanafunzi wenye usonji, wenye ulemavu wa akili, wasioona, wenye uoni hafifu, viziwi, walemavu wa viungo na wenye ualbino, wenye vipawa na vipaji pekee na wale wenye matatizo ya ujifunzaji," alisema.

Silinde alisema Januari, mwaka huu, serikali ilianzisha mpango wa kitaifa wa kubainisha watoto wenye uhitaji maalum na kubaini zaidi ya watoto 28,690 wenye aina tofauti ya uhitaji maalum.

"Hapa nilifahamishwa kuwa ninyi maofisa elimu maalum mlihusika katika zoezi hilo muhimu, ambapo wazazi na walezi wa watoto hao waliobainika kuwa na uhitaji maalumu kushauriwa na kufanikisha kuwaandikisha katika shule zilizo karibu na makazi yao kulingana na aina ya ulemavu wa mtoto husika.

"Hivyo basi ninawaomba fuatilieni hilo na kuhakikisha watoto wote waliobainishwa wameandikishwa shule husika na wanapata huduma za kielimu ikiwa ni pamoja na kupatiwa afua stahiki muhimu," alisema.

Pia aliwataka maofisa elimu hao kupata taarifa za takwimu za wanafunzi, ikiwa na vifaa maalum vya kujifunza na kufundishia na visaidizi, miundombinu na walimu wataalamu kwa kuzingatia tofauti ya makundi yaliyopo ya wanafunzi wenye uhitaji maalum.



# Mpango huduma endelevu wa maji waandaliwa sasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa Maji mkoani Mbeya, serikali na Shirika la Maendeleo la Watu wa Ujerumani (GIZ), wameanza kuandaa Mpango wa Usalama wa Maji utakaowezesha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya kutoa huduma bora na endelevu ya maji.

Wadau hao wakiongozwa na maofisa kutoka Wizara ya Maji, wamekutana jijini hapa kwa lengo la kuandaa mpango huo wa maji ambao utawahakikishia wananchi huduma ya uhakika ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Mkemia Mwandamizi kutoka Wizara ya Maji, Stanley David, alisema jana kuwa wapo hapa kuandaa mpango wa usalama wa maji kwa lengo la kuhakikisha jitihada za serikali kuwapatia wananchi huduma za majisafi na salama zinafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Wizara inaendelea kukagua na kuhakikisha usalama wa maji unaanzia kwenye chanzo cha maji hadi kwa watumiaji na kutatua matatizo yanayowakabili," alisema David.

Mwakilishi wa GIZ, Samwel Sudi, shirika la hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Maji linatekeleza mradi kusaidia Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Mbeya, Songwe na Tunduma kuandaa mpango wa usalama wa maji kwa kuhakikisha zina uwezo wa kuzalisha maji yenye bora na ya kutosha.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya UWSSA), John Nkana, alisema mpango huo utasaidia upatikanaji wa maji kwa Jiji la Mbeya na viunga vyake.

Alisema mradi huo utajikita kuangalia usalama wa maji kuanzia chanzo cha maji, usambazaji na kutibu na kwa watumiaji ili kupunguza matatizo yanayotokana na majisafi na salama.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lupaso, Kata ya Luangwa, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wakielekea shuleni hivi karibuni huku wakiwa wamebeba vifurushi begani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wachangia ujenzi wa ofisi CHADEMA

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WANANCHI wa Kata ya Ndato mkoani Mbeya bila kujali itikadi za vyama vyao wamejitokeza kufanya harambee ya kutafuta Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Kata ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Wananchi hao wamehamasika kuchangia ujenzi wa ofisi hiyo wakikusudia ndani yake pia iwe na maktaba itakayotumiwa na wanafunzi wanaosoma shule za sekondari za kata wakati wa likizo.

Diwani Mstaafu wa Kata ya Ndato, Paulo Zambi, ndiye aliyeandaa harambee hiyo akidai inalenga pia kuleta maridhiano ya kisiasa kijijini hapo.

"Sisi wananchi wa Kata ya Ndato, kwa umoja wetu tumeamua kujenga ofisi ya CHADEMA ya kata ambayo tunakusudia iwe chachu ya maendeleo kwenye kata yetu.

Ofisi hii itakuwa na jengo la ghorofa na ndani yake tunataka kuanzisha maktaba itakayosaidia watoto wetu kujisomea wakati wa likizo," alisema Zambi.

Alisema ofisi hiyo inachangiwa na wanachi wote bila kujali itikadi zao za kisiasa kwa lengo la kuleta umoja na maridhiano ya kisiasa baina ya wakazi wa kata ya Ndato.

"Maeneo mengi nchini watu wamekuwa wakifanya siasa za kuhasimiana, lakini sisi hapa kwetu tunahitaji kuondoa hiyo dhana kwani siasa ni kama imani ambayo kila mtu anaweza kuwa na imani yake, lakini bado mkakaa pamoja mkafanya mambo ya kimaendeleo," alisema Zambi.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kata ya Ndato, Mussa Pimba, alisema wamejiwekea malengo ya kukamilisha ujenzi wa ofisi hiyo ndani ya kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa.

"Tumeamua kuanza kazi hii kwa kuchangishana fedha sisi wenyewe.

Kutokana na hamasa pamoja na mwamko wa wananchi, tunaamini kuwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu ijayo tutakuwa tumekamilisha ofisi yetu na imeanza kutumika," alisema Pimba.

Mgeni rasmi kwenye harambee hiyo, mfanyabiashara Daud Nyasa, ambaye alichangia Sh. 500,000 na kutaka ofisi hiyo itakapokamilika iwe kitovu cha demokrasia ndani ya kata hiyo.

"Tunajenga ofisi hii kwa umoja wetu na tunatumia nguvu zetu wenyewe, hivyo punde itakapokamilika inapaswa kuwa kitovu cha demokrasia na haki kwa wananchi wote na sio kutumika kuwanyanyasa wananchi kwa namna yoyote ile," alisema Nyasa.

Alisema endapo ofisi hiyo itatumika ipasavyo kwa kuhakikisha haki ya kidemokrasia inatendeka, itakuwa mfano wa kuigwa nchi nzima na huwenda watu wakafika kwenye kata hiyo kujifunza kutokana na umoja, mshikamano na haki inayofanywa na wananchi wa kata hiyo.

# Abiria wahimizwa kujikinga na corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ABIRIA wanaotumia usafiri wa umma jijini Mbeya wametakiwa kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona ikiwamo kuepuka magari ambayo yamejaa ili kupunguza msongamano.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Daud, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumza na Nipashe kuhusu hatua ambazo mamlaka hiyo inachukua kukabili ugonjwa huo.

Daudi alisema pamoja na jitihada za kuhamasisha abiria kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwenye vyombo vya usafiri kunakwamishwa na uhaba wa vyombo vya usafiri nyakati za usiku.

Alitolea mfano baadhi ya maeneo ambayo yanakumbwa na uhaba wa magari nyakati za usiku kuwa ni pamoja na njia ya Mbalizi-Stendi Kuu, Mbalizi-Kabwe na kwamba hali hiyo ni hatari kwa kuwa inasababisha msongamano wa watu.

"Asubuhi watu wanaenda kwenye shughuli zao na jioni wanarejea nyumbani. Kwa kuwa wakati huo watu wanakuwa wengi na baadhi ya madereva wakishapata malengo ya siku wanaenda kuegesha magari yao, hivyo kusababisha abiria usumbufu kwa abiria muda wa usiku," alisema Daudi.

Hata hivyo, alisema LATRA imechukua hatua ya kuwahamasisha madereva na wamiliki wa vyombo hivyo kuendelea kufanya kazi nyakati za usiku ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi kwa kuwa leseni yao inawaruhusu.

"Pamoja na yote hayo bado tunawahimiza abiria kuendelea kuchukua tahadhari kwenye mabasi kwa kuhakikisha wanavaa barakoa, kunawa mikono na wao madereva na makondakta kuhakikisha abiria wanafuata maelekezo yote ya wataalamu wa afya kabla ya kupanda kwenye vyombo vyao," alisema Daudi.

Nao baadhi ya wananchi jijini Mbeya walisema wanakumbana na adha ya kupata usafiri nyakati za usiku na asubuhi ndio maana wanashindwa kufuata baadhi ya maelekezo ya wataalamu ya kuhakikisha wanakaa umbali kati ya mtu mmoja na mwingine.

Mmoja wa wananchi hao, Selina Uswege, mkazi wa Mbalizi, alisema baadhi ya wamiliki wa daladala jijini Mbeya huwa hawataki magari yao yatembee usiku hivyo huwa wanawahi kuyaegesha na hivyo kusababisha upungufu wa magari.

Alisema hali hiyo huwa inasababisha watu kusongamana kwenye magari machache ambayo huwa yanafanya kazi hata usiku na baadhi hulazimika kujazana kwenye bajaji.

"Tunaomba serikali iweke utaratibu mzuri wa kusimamia hali hii ya usafiri, hata kama ugonjwa huu tunajihami nao kwa kunawa mikono na kuvaa barakoa lakini kwenye daladala hali si nzuri," alisema.



# Jamii yatakiwa kujali wenye mahitaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, amesema ni jukumu la watu wote ndani ya jamii, kusaidia ipasavyo huduma kwa watoto yatima na wenye mahitaji maalum visiwani humo.

Aliyasema hayo jana alipotembelea kituo cha kulelea watoto yatima cha Magomeni Wandras, mjini Unguja, familia yenye watoto wanne wenye ulemavu iliyopo Kiboje, Wilaya ya Kati na Pongwe Mwera, Wilaya ya Magharibi.

Alisema watoto hao wanamahitaji makubwa yakiwamo ya makazi, chakula, malazi, na ya msingi ikiwamo huduma za elimu, huku familia zao zikikosa uwezo huo.

Alitoa wito kwa wadau na jamii hasa wenye uwezo kutoka ndani na nje ya Tanzania kujitolea kusaidia ipasavyo mahitaji ya watoto hao ili kupata huduma muhimu za kibinadamu na kuishi vyema kama binadamu wengine wote.

Alitoa wito kwa viongozi mbalimbali kuunga mkono juhudi za serikali na taasisi mbalimbali, kuhakikisha wanawatembelea watoto wa aina hiyo, ili kuona changamoto mbalimbali za mahitaji yao na kuwasaidia.

Alisema watoto yatima na wenye mahitaji maalum ni wazi wana mazingira magumu ya kuishi kwa kukosa huduma bora za msingi na kwamba kupatiwa misaada kutawapa nafuu ya maisha yao.

Akitoa mfano wa familia yenye watoto wenye ulemavu wanne ya huko Kiboje ambao kwa sasa wanalala chumba kimoja na mama yao mzazi kutokana na ukosefu wa makazi alisema: "Kuna haja kubwa ya jamii kuiona changamoto hii na kuisaidia familia hii na jambo hili sio zuri hata kimaadili hasa ukilinganisha watoto hawa ni wa kiume na wengine wana umri zaidi ya miaka 25, kulala na mama yao sio busara."

Aliwataka watu wenye uwezo kuguswa moja kwa moja na tatizo hilo na kuhakikisha kwamba wanatoa msaada wa mahitaji kwa familia za aina hiyo.

Katika ziara hiyo aliwafariji watu hao wanaoishi katika mazingira magumu kwa kutoa misaada mbalimbali ya chakula, sabuni na fedha taslimu kupitia Jumuiya ya Kuwasaidia Watoto Yatima na wenye Mahitaji Maalum (ZAYOTH).

# Z'bar yapata mgao wa bil. 1.6/- wa makusanyo tozo ya miamala

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema tayari jumla ya Sh. bilioni 1.66 zimekusanywa kwa ajili ya tozo ya miamala ya simu ambazo zitatumika kwa upande wa Zanzibar katika matumizi mbalimbali yenye lengo la kusaidia miradi ya maendeleo na ustawi wa jamii.

Alisema hayo katika mkutano wa Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zanzibar ambao wanaendelea na vikao vya kujadili changamoto za Muungano.

Viongozi hao juzi walitembelea miradi miwili ya ujenzi wa jengo la kisasa la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume pamoja na Kiwanda cha Maziwa kilichoko Fumba Mkoa wa Magharibi Unguja.

Viongozi hao wameridhika na hatua zinazoendelea katika maeneo hayo ya utoaji wa huduma katika maeneo hayo.

Waziri Nchemba alisema fedha hizo ni matokeo ya utekelezaji wa sheria iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ya tozo ya miamala ya simu ambayo lengo lake kubwa ni kuongeza mapato ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema licha ya kuwapo kwa mashinikizo mbalimbali kuhusu tozo za miamala ya simu, faida za makusanyo ya fedha zimeanza kuonekana kwa taifa na wananchi kwa ujumla kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Niwajulishe wananchi wa Zanzibar kwamba tozo zinazotokana na miamala ya simu ambazo zimepitishwa kwa mujibu wa sheria za Bunge la Jamhuri ya Muungano na kuanza kutozwa Julai, matunda yake yameanza kuonekana ambapo kwa upande wa Zanzibar imepata mgao wa Sh. bilioni 1.66 ambazo hizo zitakabidhiwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupanga matumizi yao," alisema.

Waziri Nchemba alisema miongoni mwa changamoto za Muungano ambazo tayari zimepatiwa ufumbuzi ni suala la Zanzibar kuomba mkopo na misaada katika taasisi za fedha za kimataifa.

Alisema kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria ya Fedha na Mikopo ya Nje, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo huru kukopa katika taasisi za fedha za kimataifa na nchi binafsi. Hatua hiyo itaiwezesha Serikali ya Zanzibar kukopa fedha katika taasisi za kifedha na kibenki kwa ajili ya shughuli wanazozitaka za kipaumbele.

"Zipo changamoto za Muungano ambazo wengine wanazita kero katika sekta ya fedha na mikopo katika taasisi za fedha za kimataifa tumezipatia majibu yake ambapo sasa Zanzibar rukhsa kukopa katika taasisi za kifedha kama ambavyo mlimuona Waziri wa Fedha wa SMZ akizungumza na ujumbe wa Benki ya Dunia," alisema.

Pia alisema matumizi ya fedha ya shughuli za uhamiaji zinazopatikana Zanzibar yalikuwa yanaidhinishwa na Bunge sasa yatatumika visiwani humo.

"Tumejadili kuhusu kodi ya ongezeko la thamani na mwananchi alikuwa akitozwa kodi mara mbili iwapo atatoa bidhaa Bara, hivyo ukitoa upande mmoja wa Muungano iwe imeshamaliza," alisema.

Alisema wanaendelea kurekebisha maeneo mengine ambayo yanachangamoto kwa sababu Muungano ni wa kidugu hivyo pande zote wafanye shughuli zao za kiuchumi na kimaendeleo bila ya vikwazo.

Akieleza changamoto katika Kiwanda cha Maziwa Azam, Mkuu wa Ubora wa Bidhaa wa kiwanda hicho, Tumaini Fredric, alitaka serikali kupunguza kodi ili kukipa uwezo kiwanda hicho kuzalisha maziwa badala ya kupata hasara kubwa.

Alisema kiwanda hicho kilisita kuzalisha bidhaa ya maziwa kutokana na changamoto nyingi ikiwamo kodi kubwa wanayotozwa na Serikali ya Tanzania kwa lita moja hutakiwa kuilipia Sh. 250 ambayo ni kubwa.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha lita 180,000 kwa siku na sasa kinazalisha tani 5,000 wakati miaka mitatu iliyopita ilikuwa inazalisha tani 26,000.

Naye Mkurugenzi wa uratibu wa shughuli za Muungano, Siajabu Suleiman Pandu, alisema kikao hicho ni muhimu ambacho kinatokana na ushauri wa viongozi wakuu akiwamo Rais wa Jamhuri ya Muungano Samia Suluhu Hassan kuona kero za Muungano zinapatiwa ufumbuzi na kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo fedha.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya pamoja ya Serikali ya Muungano ya Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), wanaoshughulikia masuala ya Muungano, wakisikiliza maelezo kuhusu changamoto za upatikanaji wa maziwa kutoka kwa Mkuu wa Viwango vya Bidhaa katika Kiwanda cha Maziwa cha Azam, Tumaini Fredrik (kushoto), walipofanya ziara kiwandani hapo, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 25 matatani kufanya biashara bila leseni

**Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WATU 25 wakiwamo mameneja mauzo wa baa wamekamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kufanya biashara bila ya leseni katika operesheni iliyoendeshwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo Zanzibar, Abdulrazaki Abdulkadiri na askari waliokuwa na silaha za moto usiku wa Agosti 22 katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Watuhumiwa hao wamesomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Malindi, Mwanahidi Abdalla Othman, wakiwamo wanaume saba na wanawake 18 na wote walikana mashtaka yao isipokuwa mmoja alikiri kosa na kutakiwa kulipa faini ya Sh. 800,000.

Mwendesha mashtaka kutoka Jeshi la Polisi, Suleiman Masoud, alisema watuhumiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kufanya biashara ya vileo bila kuwa na leseni kitendo ambacho ni kinyume na Sheria ya Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar Namba 9 ya mwaka 2020.

Hata hivyo, Hakimu Mwanaidi Abdalla Othman, alisema dhamana kwa watuhumiwa ipo wazi kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili wenye vitambulisho, fedha taslimu Sh. 200,000 na dhamana ya maandishi Sh. 300,000 kabla ya kupandisha dhamana ya fedha taslimu kufikia Sh. 400,000 kwa kila mshtakiwa. Wakili wa watuhumiwa, Alex Paul, alipinga na kuomba mahakama kuangalia upya masharti ya dhamana kwa madai haiwezekani shtaka moja masharti ya viwango vya dhamana yawe tofauti na kuwapa wakati mgumu washtakiwa.

Hakimu Mwanaidi alisema kesi hizo zitaendelea kutajwa kwa washtakiwa kwa tarehe tofauti kwa kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka na washtakiwa baada ya kukuna mashtaka dhidi yao.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kiongozi Mwandamizi wa Jumuiya ya Wauza Vinywaji Zanzibar, Hussen Ali Kimti, alisema wamesikitishwa na Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar kuvunja amri ya Mahakama Kuu ya kusitisha utekelezaji wa tozo mpya ya leseni za baa mpaka kesi ya msingi walioifungua kumalizika visiwani humo.

Alisema baada ya Sheria namba tisa ya Bodi ya vileo ya mwaka 2020 kuanza kutumika Jumuiya ya wauza vileo Zanzibar iliamua kufungua kesi ya kupinga tozo za leseni kwa kupandishwa kwa zaidi ya asilimia 200 bila ya kushirikishwa wadau katika sekta hiyo.

"Tulifungua kesi kupinga tozo ya leseni kupandishwa kutoka milioni mbili hadi milioni 4.8 kwa kila baa na masharti ya baa ziwe umbali wa mita 1,000 kutoka maeneo ya huduma za jamii kama shule, nyumba za ibada hospitali na makazi, sisi tunaona baa zote zitafungwa kwa mujibu wa sheria hii na watu kupoteza ajira," alidai Kimti.

Alisema kupitia kesi namba moja ya mwaka 2021 chini ya Jaji Fatma Hamid, Jumuiya hiyo dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi aliwataka kusitisha utekelezaji wa tozo mpya za leseni hadi kesi ya msingi itakapomalizika, lakini bodi hiyo imeshindwa kuheshimu.

Alisema mamlaka za serikali zinatakiwa kuheshimu mihimili mitatu ya dola, Serikali, Baraza la Kutunga Sheria na Mahakama, lakini kitendo cha kuwakamata mameneja mauzo wa baa na kuwashtaki wakati kuna zuio la mahakama ni kutoheshimu muhimili huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**A SALES PERSON IS REQUIRED**

A SALES PERSON IS REQUIRED FOR AN ESTABLISHED PHARMACEUTICAL COMPANY BASED IN DAR ES SALAAM

**CONTACT: 0713 786 300**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JONATHAN MBUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4598-0164** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MAKOKA mwaka 2013, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/29634/2020**

1164209 02


## KUPOTEA KWA VYETI



**DISMAS NEVAGIRI SOKA** anatangaza kupotelewa na vyeti ,cha kidato cha nne index namba S0485-0235kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MAJENGO mwaka 2013,na cheti cha diploma chuo cha **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY index namba DSM/DMPR/15/32330** mwaka 2017,na certificate ya chuo cha **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY** yenye index namba **DSM/BTCMPR/14/19094** mwaka 2015, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/KIL/RB/409697/2021**

1164211 02

## KUPOTEA KWA CHETI



**SIXTUS KAMANDA IGNACE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1045/0349** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **DAR ES SALAAM mwaka 2011,**yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CEN/ RB/396992/2021**

1164193 02

## KUPOTEA KWA CHETI



**TUNGARAZA BENEDICTO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0208/0003** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary KIPINGO mwaka 2014, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisis Polisi taarifa **DAR/UR/RB/413736/2021**

1164212 02

## ENEO LA UWEKEZAJI LINAUZWA

LIPO KIBAHA, KONGOWE CENTRE. NI EKARI NNE,KUNA MAJENGO,UMEME NA MAJI VIPO,LINA HATI

**MAWASILIANO:**
**0713 515744**
**0657 585952**

1164213 02

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**N0 237/2021**

Ombi la S**AMWELI KAPAYA SAFISHA** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **PASCHAL GRACEFORD SAFISHA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 24/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 9/08/2021**

1164218 02

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha KINGOLWIRA**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 21/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU TATU HAMISI NGULUMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JASMINI HAMISI NGULUMA**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 mwezi 09 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakama kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 23 mwezi 08 Mwaka 2021
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 9/08/2021**

1164219 02

---

## TANGAZO KUPOTEA KADI YA GARI

**Edward Lassa Maduhu** Mkazi wa Mwasele Manispaa ya Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T. 754 CBF** aina ya Mitsubishi injini namba **6D177950.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu, au awasiliane na Edward Lassa Maduhu kwa simu namba **0767872779.** Rb namba: Shy/Rb/2021, Control namba **9910830025719.**

1164220 02

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF ILEMELA DISTRICT**
**AT ILEMELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 9 OF 2021**
**In the matter of Estate of the late PENINA OSCAR NAVETA**
**AND**
**In the matter of Application for Grant of Letter of Administration by KENEDY GERSHON CHIGURU**
**GENERAL CITATION**
**{RULE 75}**

All persons clamming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant for letters of probate and Administration is made to the above named petitioner.
Caveat/objection to the grant should be filed on or before 3rd Day of SEPTEMBER,2021.
Date at mwanza this 11 day of AUGUST,2021

.................................................
**DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE**
**ILEMELA- MWANZA**

1164223 02

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 105 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU DR.COL.MOSES BEATUS MLULA MWOMBAJI COL.HOJA SIMON NGW'ESHEMI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuhudhuria mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 mwezi 09 mwaka 2021

**Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 17 mwezi 08 mwaka 2021**

NAIBU MSAJILI

1164224 02

---

## FOR SALE



Embassy of the State of Qatar in Dar es Salaam would like to sale **2012 TOYOTA HILUX PICK-UP in a mint condition.**

Interested buyers can view the vehicle between **0900-1500 at the Embassy located at 6 Msasani Road, Dar es salaam.**

**CONTACT: 0715 556056**

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Zuma achangisha fedha kugharamia kesi yake

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma, anauomba umma kumchangia fedha zitakazomwezesha kukabiliana na kesi inayomkabili ya tuhuma dhidi ya rushwa.

Katika kurasa rasmi ya twitter ya taasisi yake imewataka raia wa Afrika Kusini na duniani kote, kumshika mkono kwa kuchangia fedha zitakazoweza kumsaidia kulipia gharama za wakili.

Ujumbe huo umeambatana na namba ya akaunti ikiwa na jina la JG Zuma. Zuma anatumikia kifungo cha miezi 15, tangu aliposhtakiwa kwa kuidharau mahakama kwa kushindwa kufika mahakamani.

Zuma alikuwa amelazwa hospitalini mapema mwezi huu, hivyo kuchelewesha kuanza kusikilizwa kwa kesi yake dhidi ya tuhuma za rushwa. **BBC**

## UN yaitaka Taliban kuheshimu haki za wanawake

**Kabul,** AFGHANISTAN

MKUU wa Masuala ya Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa Michelle Bachelet, ameelezea wasiwasi mkubwa kuhusu hali ya Afghanistan, baada ya Wataliban kuingia madarakani, akisema jinsi wanavyowashughulikia wanawake huenda yakaashiria kuvuka mstari mwekundu.

Akizungumza katika kikao cha dharura kuhusu Afghanistan, Bachelet amewahimiza Wataliban kutimiza ahadi za kuheshimu haki za wanawake na wasichana, makundi ya kikabila na kidini ya walio wachache, na kujizuia kulipiza kisasi.

Bachelet ameliambia baraza hilo kwamba, Wataliban wanapaswa kuweka upya mshikamano wa kijamii na maridhiano, pamoja na kuheshimu haki za wale wote waliotaseka wakati wa miongo mingi ya vita. **DW**

# Hichilema aapa, aitaka sekta binafsi kukuza uchumi

**Lusaka,** ZAMBIA

KIONGOZI mkongwe wa upinzaji Zambia, Hakainde Hichilema ameapishwa kuwa rais huku akiinua matumaini kwa wanasiasa wengine wa upinzani katika mataifa ya Kiafrika, kwamba wao pia wanaweza kuingia madarakani.

Hichilema amekula kiapo kuwa rais wa Zambia mbele ya umati wa watu waliokuwa wakishangilia kwenye uwanja wa Mashujaa katika mji mkuu, Lusaka.

Akizungumza baada ya kula kiapo, kwenye hotuba ya kwanza kwa taifa lake, aliwaambia Wazambia kwamba wakati wa mabadiliko umewadia akisema uchumi utakua huku akiomba ushirikiano wa sekta binafsi.

Sherehe za uapisho zimehudhuriwa na wakuu kadhaa wa nchi pamoja na viongozi wa vyama vya upinzani kutoka barani Afrika.

Mwanasiasa huyo wa upinzani mwenye umri wa miaka 59 alishinda uchaguzi kwa kura nyingi wiki iliyopita.

**Utawala wake utaangazia masuala ya madini, nishati, ardhi na utalii huku akimshukuru mtangulizi wake Lungu, kwa aliyoyafanya.**

Mwandishi wa BBC Nomsa Maseko alisema wananchi wengi wanamtarajia kiongozi huyo mpya kuboresha hali ya maisha yao, ikiwamo nafasi za ajira, kupambana na ufisadi na kuboresha uchumi.

Rais Hichilema alimshinda rais aliyeondoka madarakani Edgar Lungu katika uchaguzi uliofanyika wiki chache zilizopita.

Kati ya marais waliohudhuria sherehe hzio ni Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan, Mokgweetsi Masisi (Botswana), Cyril Ramaphosa (Afrika Kusini) na Emmerson Mnangagwa wa Zimbabwe.

### HOTUBA YA MATUMAINI

Hichilema akizungumza baada ya kula kiapo, kwenye hotuba ya kwanza kwa taifa lake, aliwaambia Wazambia kwamba wakati wa mabadiliko umewadia akisema uchumi utakua huku akiomba ushirikiano wa sekta binafsi.

Alisema uwekezaji ni muhimu kuanzia ngazi ya chini na kila mkoa badala ya kusubiria wawekezaji kutoka Ulaya.

Aliahidi mambo makuu matatu ikiwamo uhakika wa chakula, akisema: Hakuna Mzambia atakayelala bila shibe."

Alisema utawala wake utaangazia masuala ya madini, nishati, ardhi na utalii huku akimshukuru mtangulizi wake Lungu, kwa aliyoyafanya.

"Demokrasia imeingia Zambia, kwa Waafrika na duniani."

Alisema serikali yake itapambana na rushwa akisema baraza la mawaziri litakuwa na uwakilishi wa nchi nzima na kila mkoa utapata kiwango sawa cha maendeleo mapya.

Hichilema alisema katika utawala wake vyombo vya habari watajiona wapya kutokana na kufanya majukumu yao kwa uhuru.

"Elimu ndio uwekezaji muhimu kwa mtoto na wa kipekee, mimi ni mfano." Alitoa wito kwa Wazambia kuungana kujenga taifa. **BBC**



Rais Hakainde Hichilema akipokea heshima ya kijeshi kama mkuu wa majeshi Zambia, katika Uwanja wa Mashujaa Lusaka, jana. **PICHA: BBC**

# Rais Uhuru Kenyatta amtaka Ruto kujiuzulu

**Nairobi,** KENYA

RAIS wa Kenya Uhuru Kenyatta, amemtaka makamu wake, William Ruto aliyehudumu naye kwa miaka tisa, kujiuzulu badala ya kuishambulia serikali ambayo wanaitumikia.

Rais Kenyatta aliyeonekana kuhamaki aliyasema hayo kwa mara ya kwanza tangu, Mahakama ya Rufani kutupilia mbali, Mpango wa Maridhiano wa Taifa - BBI, uliolenga kubadilisha Katiba kwa kuitaja kuwa iliyokiuka sheria.

Matamshi yake kwa mara nyingine yakiongeza kaa la moto, kati yake na makamu wake William Ruto, ulioanzishwa na ushirikiano wake na kiongozi wa ODM Raila Odinga.

Kenyatta, alimkosoa makamu wake ambaye amekuwa mkosoaji mkuu wa serikali, ambaye alisema anawachanganya wapigakura kwa matendo yake.

Ruto amekisajili chama chake cha United Democratic Alliance, licha ya kuwa katika chama tawala cha Jubilee na kubainisha kuwa atagombea kiti cha urais.

"Kitu cha heshima cha kufanya ni kujiuzulu na kuruhusu wanaotaka kuendelea, kisha ufikishe ajenda yako kwa wananchi, jambo ambalo hufanyika katika mazingira ya demokrasia. Kwa upande mmoja huwezi ukasema huondoki na wakati huo huo unasema sikubaliani."

Huku akimuunga Ruto kwa kuunda msingi wa siasa za mwaka ujao kuwa haki yake ya kikatiba, Rais Kenyatta alimkosoa kuhusu njia anayotumia kufikia malengo hayo.

Kenyatta amebainisha kuwa hatayumbishwa na misukosuko inayoshuhudiwa katika kutimiza malengo yake.

Rais Kenyatta ambaye anakamilisha utawala wa mihula ya miwili ya miaka kumi, amepuuzilia mbali mjadala wa kuahirisha tarehe ya uchaguzi mwakani, huku washirika wake wa karibu wakimsihi kubakia madarakani.

Uchaguzi mkuu ujao utafanyika tarehe 9, Agosti, mwaka 2022. Mahakama ilipotengua Mpango wa Maridhiano wa Taifa, rais alisema kuwa ni Wakenya walipoteza, huku Ruto akisherehekea ushindi huo.

"Uamuzi wa Mahakama, unadhihirisha kuwa taifa la Kenya, linaongozwa kwa misingi ya sheria, sio misingi ya binadamu."

Matamshi ya rais yanajiri huku Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia Joe Mucheru, akimshambulia Ruto kwa kutoa ahadi kwa vijana na kutumia injili kuwashawishi wananchi. **DW**

MECHI KALI
HOME
AWAY
WEST BROMWICH
3.43 | 3.48 | 2.01
ARSENAL

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 450

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
halopesa

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SHAQIRI ATUA LYON KWA PAUNI MIL. 9.5



**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imekubali dau la pauni milioni 9.5 kutoka Lyon kwa ajili ya kumuuza kiungo mshambuliaji wa Uswisi, Xherdan Shaqiri, baada ya kushindwa kukubaliana Januari.

Klabu hizo zimekubaliana ada kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 na Lyon ilithibitisha Jumapili kwamba, atafanya vipimo vya afya jana. Shaqiri ameshakubaliana maslahi binafsi na Lyon na taarifa zinasema atasaini mkataba wa miaka minne utakaomweka hapo hadi mwaka 2025.

"Olympique Lyonnais inafurahi kuwa hatimaye imefikia makubaliano na Liverpool kwa uhamisho wa kiungo wa kimataifa wa Uswisi, Xherdan Shaqiri," ilisema taarifa kwenye tovuti ya Lyon.

"Shaqiri, ambaye atawasili Lyon usiku wa leo (jana) atakaribishwa na Juninho. Kukamilisha uhamisho huo kunabaki kwenye vipimo vya afya ambapo akifaulu atakamilisha taratibu za mwisho za kiutawala."

Shaqiri aliweka wazi nia yake ya kuondoka Liverpool msimu huu wa majira ya joto kutafuta nafasi ya kucheza.

Anaondoka akiwa amecheza mechi 63 kwa klabu ya Liverpool tangu ajiunge kutoka Stoke City mwaka 2018, na ametwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super, Klabu Bingwa Dunia na Ligi Kuu England.



# *Kimmich ajifunga Bayern Munich*

**MUNICH,** Ujerumni

JOSHUA Kimmich ameongeza mkataba wake na Bayern Munich utakaomweka hapo hadi mwaka 2025, kwa mujibu wa tovuti ya klabu hiyo.

Akiwa na uwezo wa kucheza kwenye safu ya kiungo au beki wa pembeni, Kimmich alijiunga na klabu hiyo kutoka RB Leipzig mwaka 2015 na amefanikiwa kushinda mataji 17 na Bayern, ambao wanatafuta taji la 10 mfululizo la Ligi Kuu ya England, Bundesliga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alisema sababu muhimu zaidi ya kuongezwa kwa mkataba wake ni kufuata mapenzi yake kwa furaha kila siku huko Bayern.

Kimmich aliongeza kuwa: "Juu ya hayo, familia yangu inahisi iko nyumbani hapa. Munich imekuwa nyumba ya pili."

Ana taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya aliloshinda mwaka 2020, na mataji sita ya Bundesliga mfululizo kutoka 2016 hadi 2021.

Kimmich amefunga mabao 30 na pasi za mwisho 73 katika michezo 264 ya Bayern Munich hadi sasa.

## HABARI MICHEZO


,150,500

# JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/08/21 | 17:00 | Brighton vs Everton | 2.31 | 3.27 | 3.16 |
| 02. 28/08/21 | 17:00 | Newcastle vs Southampton | 2.60 | 3.40 | 2.65 |
| 03. 28/08/21 | 17:00 | Huddersfield vs Reading | 2.42 | 3.20 | 2.86 |
| 04. 28/08/21 | 17:00 | Preston vs Swansea | 2.46 | 3.26 | 2.77 |
| 05. 28/08/21 | 17:00 | Luton Town vs Sheffield Utd | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 06. 28/08/21 | 18:00 | Celta Vigo vs Athletic Bilbao | 2.42 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 28/08/21 | 19:30 | Liverpool vs Chelsea | 2.45 | 3.36 | 2.86 |
| 08. 28/08/21 | 20:30 | Real Oviedo vs Tenerife | 2.60 | 2.85 | 2.95 |
| 09. 29/08/21 | 16:00 | Burnley vs Leeds | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 10. 29/08/21 | 16:00 | Angers vs Rennes | 2.85 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 29/08/21 | 16:30 | Union Berlin vs Monchengladbach | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 12. 29/08/21 | 20:30 | Cadiz CF vs Osasuna | 3.01 | 3.01 | 2.56 |
| 13. 29/08/21 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Granada | 2.61 | 3.22 | 2.77 |


MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 25 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1056 | Consadole Sapporo vs Nagoya Grampus | 2.37 | 3.00 | 2.95 |
| 13:00 | 1240 | Urawa Red Diamonds vs Sanfrecce Hiroshima | 2.81 | 3.15 | 2.37 |
| 13:00 | 1747 | Shimizu S Pulse vs Kashima Antlers | 3.96 | 3.53 | 1.79 |
| 13:00 | 2532 | Yokohama vs Gamba Osaka | 3.29 | 3.19 | 2.09 |
| 13:00 | 2788 | Vegalta Sendai vs FC Tokyo | 3.78 | 3.49 | 1.84 |
| 13:00 | 2968 | Sagan Tosu vs Yokohama F Marinos | 4.05 | 3.96 | 1.68 |
| 13:00 | 3165 | Cerezo Osaka vs Shonan Bellmare | 1.79 | 3.38 | 4.16 |
| 13:00 | 3396 | Oita Trinita vs Vissel Kobe | 3.96 | 3.24 | 1.87 |
| 13:00 | 3642 | Tokushima Vortis vs Kashiwa Reysol | 2.57 | 2.96 | 2.72 |
| 13:00 | 4402 | Avispa Fukuoka vs Kawasaki Frontale | 7.14 | 4.44 | 1.37 |
| 13:00 | 5766 | Jeonbuk Hyundai vs Pohang Steelers | 1.92 | 3.24 | 3.78 |
| 13:30 | 1600 | Incheon Utd vs Daegu | 3.20 | 3.35 | 2.07 |
| 13:30 | 5489 | FC Seoul vs Ulsan Hyundai | 4.07 | 3.05 | 1.92 |
| 14:00 | 5603 | Suwon Samsung vs Suwon City | 2.36 | 3.10 | 2.86 |
| 14:45 | 5302 | Geylang Int. vs Tampines | 3.70 | 3.89 | 1.76 |
| 16:00 | 1536 | Ararat Armenia vs Artsakh | 1.52 | 3.87 | 5.61 |
| 16:00 | 3576 | SuperSport Utd vs Golden Arrows | 2.16 | 2.71 | 4.04 |
| 18:00 | 2222 | Banik Sokolov vs Bohemians | 9.74 | 6.62 | 1.19 |
| 18:00 | 2658 | Bloemfontein Celtic vs Cape Town City | 2.70 | 2.95 | 2.70 |
| 18:00 | 3788 | SK Benesov vs Teplice | 8.14 | 5.81 | 1.25 |
| 18:00 | 3819 | Amazulu vs Moroka Swallows FC | 2.54 | 2.69 | 3.18 |
| 18:00 | 3847 | Kromeriz vs Zbrojovka Brno | 5.42 | 4.16 | 1.49 |
| 18:00 | 4346 | Hlucin vs Banik Ostrava | 9.68 | 6.58 | 1.19 |
| 18:00 | 4528 | SK Nova Dedinka vs Raca Bratislava | 8.20 | 6.00 | 1.30 |
| 18:00 | 5138 | Stellenbosch vs TS Galaxy FC | 2.42 | 2.66 | 3.44 |
| 18:00 | 5359 | Kaizer Chiefs vs Baroka FC | 1.79 | 2.89 | 5.68 |
| 18:00 | 5633 | Unicov vs Sigma Olomouc | 9.69 | 7.56 | 1.16 |
| 18:00 | 5692 | TJ Tatran Sedlcany vs Ceske Budejovice | 19.35 | 8.90 | 1.07 |
| 18:15 | 4864 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs Ajman Club | 1.34 | 5.03 | 6.58 |
| 18:15 | 5573 | Ittihad Kalba vs Jazira Abu Dhabi | 6.20 | 4.84 | 1.38 |
| 18:30 | 2017 | FF Jaro vs EIF Ekenas | 2.05 | 3.39 | 3.20 |
| 19:00 | 5263 | FK Stechovice vs Varnsdorf | 4.56 | 3.88 | 1.62 |
| 19:05 | 2330 | Al Raed Club vs AL Hazm | 2.02 | 3.72 | 3.28 |
| 19:30 | 5244 | FK Zbuzany vs Slovan Liberec | 6.60 | 5.24 | 1.33 |
| 20:00 | 2922 | Ghazl EL Mahallah vs Arab Contractors | 3.30 | 2.76 | 2.44 |
| 20:30 | 3767 | Al Ain vs Emirates Club | 1.32 | 4.56 | 8.53 |
| 21:00 | 1143 | Hafnarfjordur vs Keflavik IF | 1.51 | 4.26 | 5.04 |
| 21:00 | 3497 | KA Akureyri vs Breidablik | 3.64 | 3.34 | 1.92 |
| 21:00 | 4244 | Antofagasta vs CD Palestino | 2.52 | 2.96 | 2.77 |
| 21:00 | 5907 | IA Akranes vs KR Reykjavik | 6.00 | 4.64 | 1.40 |
| 21:45 | 5651 | Newport vs Southampton | 5.32 | 3.89 | 1.59 |
| 21:45 | 5807 | Newcastle vs Burnley | 1.90 | 3.45 | 3.85 |
| 22:00 | 2277 | Vila Nova GO vs Avai | 3.34 | 2.90 | 2.22 |
| 22:00 | 2495 | Brondby vs RB Salzburg | 5.61 | 4.61 | 1.50 |
| 22:00 | 2678 | West Bromwich vs Arsenal | 3.43 | 3.48 | 2.01 |
| 22:00 | 4702 | Shakhtar Donetsk vs Monaco | 2.86 | 3.31 | 2.45 |
| 22:00 | 5673 | La Equidad vs Llaneros FC | 1.46 | 3.77 | 6.95 |
| 22:00 | 5707 | Dinamo Zagreb vs Sheriff Tiraspol | 1.40 | 4.81 | 7.21 |
| 22:00 | 5740 | Misr Lel Makasa vs Pyramids | 5.34 | 3.07 | 1.78 |
| 23:30 | 1478 | Union La Calera vs Colo Colo | 3.67 | 2.95 | 2.07 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# ARSENAL WAKOMAA NA USAJILI WA AOUAR

**LONDON,** England

MWANDISHI wa Sky Sport Italia anayehusika na habari za usajili wa wachezaji, Fabrizio Romano amefichua kwamba, klabu ya Arsenal bado inavutiwa kutaka kumsajili mchezaji wa Lyon, Houssem Aouar.

'Washikabunduki' hao walishindwa kufikia makubaliano na kiungo huyo msimu uliopita wa majira ya joto, lakini Aouar sasa anapatikana kwa dau dogo la angalau pauni milioni 20.

"Kuna hali ngumu kwa upande wa wakala, na ndio sababu tutamuona Aouar hadi siku za mwisho ya dirisha kwa sababu sasa bado kuna tetesi kwa klabu kadhaa ambazo ni Tottenham na Arsenal," alisema Romano kupitia Youtube ya Don Robbie.

"Klabu hizi mbili zina nia ya kweli kwa Aouar. Arsenal kama unavyojua vizuri walimtaka na bado wanaangalia hali yake.

"Lakini sasa ni muhimu kwa Arsenal kumsajili mchezaji huyo na wanaonekana wana nia ya kweli."



# *Kompany, Silva kuwekewa sanamu Etihad*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City watawawekea sanamu, David Silva na Vincent Kompany nje ya Uwanja wa Etihad kabla ya mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal Jumamosi.

City iliagiza sanamu hizo kwa wawili hao ambao wanaonekana kama wachezaji wakubwa zaidi katika historia ya klabu hiyo na baadaye itaongeza moja ya mshambuliaji wao wa zamani, Sergio Aguero.

Kompany alitumia miaka 11 kwenye klabu hiyo, wakati Silva alikuwa Etihad kwa muongo mmoja na alisaidia kuibadilisha City kuwa moja ya timu bora nchini England.

Sanamu hizo zilizoundwa na msanii wa Uingereza, Andy Scott na zilipomalizika zilibaki kuwa siri hadi hapo zitakapowekwa wazi kwa umma wikendi hii.

Scott aliweza kukutana na Kompany na Silva kwenye studio yake huko Philadelphia nchini Marekani.

Mwenyekiti wa Man City, Khaldoon Al Mubarak alitangaza uamuzi wa kuwaheshimu wachezaji hao mwaka 2019 baada ya kuondoka kwa Kompany aliyekwenda kuwa kocha mchezaji kule Anderlecht.

"Bado ni ngumu kufahamu. Ninarudi mwanzo kabisa wakati nilisaini Man City na hatukuzungumza juu ya sanamu wakati huo," alisema Kompany akinukuliwa na BBC Sport.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI SASA KUANZA PSG, IKIIVAA REIMS JUMAPILI

●●● Lakini Ramos hatacheza mpaka baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa mwezi...

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, amesema Lionel Messi atakuwa sehemu ya kikosi kwenye mchezo wa wikendi inayokuja wakati timu hiyo itakapocheza na Reims kwenye mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Baada ya kupata ushindi wa mechi tatu mfululizo za ufunguzi, PSG sasa wapo kileleni mwa msimamo ligi hiyo na wanazidi kuimarika licha ya kukosekana kwa wachezaji kama Messi na Neymar.

**Hiyo haijaleta upungufu wowote, zaidi ni kwamba sasa timu hiyo inakwenda kupata huduma zaidi pale wachezaji hao wawili watakapoungana na timu wakati wa usajili mpya, Gianluigi Donnarumma aliweza kukaa benchi kwenye mchezo wa Ijumaa iliyopita wakishinda mabao 4-2 dhidi ya Brest.**

"Wiki imekuwa nzuri sana kwa Leo Messi, kwa hiyo tunatumaini mwishoni mwa wiki anaweza kuisadia timu na atajumuishwa kwenye kundi kwa ajili ya mchezo," alisema Pochettino akiiambia ESPN.

Wakati Achraf Hakimi na Georginio Wijnaldum wamecheza michezo yote mitatu ya PSG katika ligi hiyo baada ya kujiunga na miamba hiyo ya Ufaransa, Messi na Neymar hawajaingia uwanjani.

Messi, Donnarumma na Ramos bado hawajaweza kucheza mchezo wowote kwa PSG hadi sasa.

Pia, Ramos hatacheza mpaka baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa mwezi unaokuja.

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG KUACHWA

ARSENAL wako tayari kusikiliza ofa, kwa ajili ya nahodha wake, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, na hawatamzuia iwapo mshambuliaji huyo wa Gabon atataka kuondoka kabla ya kufungwa kwa dirisha hili la usajili. ***(Telegraph)***

### ARTETA, ARSENAL PAMOJA

ARSENAL pia imedhamiria kumuunga mkono kocha wa timu hiyo aliyeko kwenye shinikizo kubwa, Mikel Arteta kufuatia vipigo viwili ilivyovipata timu hiyo kwenye Ligi Kuu England. ***(Mirror)***

### KANE HAUZWI - TOTTENHAM

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy hatapunguza thamani ya mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, na yuko tayari hata kukataa ofa kubwa ya kuvunja rekodi ya uhamisho Uingereza inayokaribia pauni milioni 150 kutoka Manchester City. ***(Telegraph)***

### NIGUEZ HUYO CHELSEA

CHELSEA wanafikiria kumchukua kwa mkopo kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26, wakati huo huo "The Blues" hao wamewapa mikataba mipya, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28 na Andreas Christensen, 25. ***(Telegraph)***

### TORREIRA KUTUA FIORENTINA

KIUNGO wa Arsenal, Lucas Torreira mwenye umri wa miaka 25, anakaribia kutua Fiorentina kwa mkopo baada ya kuisaidia Atletico Madrid chini ya kocha Diego Simeone kushinda taji la LaLiga msimu uliopita alikokua anacheza kwa mkopo. ***(football.london)***

### RICE KUIGOMEA WEST HAM

KIUNGO wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, amepanga kukataa ofa yoyote ya kusaini mkataba mpya kutoka klabu yake ya West Ham, kama mgomo baada ya klabu hiyo kumuwekea bei ya juu na kuweka ugumu wa yeye kuhama msimu huu. ***(Mail)***

### WILLIAN HUYOOO CORINTHIANS

KIUNGO wa Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 33, yuko njiani kuondoka Arsenal bure na kujiunga na Corinthians ya nyumbani kwao, mazungumzo yako katika hatua za mwisho. ***(Mail)***

### KOUNDE KUSAJILIWA CHELSEA

CHELSEA wana matumaini ya kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde, kutoka Sevilla huku kukielezwa, kwenye mkataba wake kuna kipengele cha pauni milioni 77, ili kumruhusu kinda huyo mwenye umri wa miaka 22 kuhama. ***(90Min)***

### CAMAVINGA HAITAKI UNITED

MANCHESTER United bado inamtaka kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa angetamani kujiunga na Paris St-Germain au klabu kutoka Hispania. ***(ESPN)***

## Kagera Sugar yabeba wawili Gwambina FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imeendelea kufanya usajili kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu 2020/21, kwa kusajili wachezaji wawili wa klabu ya Gwambina FC, ambayo kwa sasa imeshuka daraja huku mmoja akitokea Namungo FC.

Wachezaji hao ambao kila mmoja aliingia mkataba wa miaka miwili na kutambulishwa jana ni straika hatari, Meshack Abraham na Yusuph Dunia wote kutoka Gwambina FC, huku ikimsajili kiungo maridadi Abeid Athumani kutoka Namungo FC.

Katibu Mkuu wa Kagera Sugar, Ally Masoud, amesema mpaka sasa wamemaliza usajili kwa asilimia 90, na wana uhakika mpaka dirisha litakapofungwa, watakuwa wamekamilisha kusajili wachezaji wote ambao wanawahitaji.

"Tumekamilisha usajili kwa asilimia 90 na tumeshaanza kutangaza. Kabla ya muda kumalizika tutakuwa tumemaliza kila kitu. Msimu huu tumesajili wachezaji mchanganyiko. Kuna wachezaji wazawa na wakigeni," alisema.

Hata hivyo, alisema mazoezi kwa ajili ya msimu mpya bado hayajaanza, lakini wachezaji wao wameshaanza kuwasili.

## Coastal yashusha nyota wa3 wakigeni

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umesema umekamilisha usajili wa nyota watatu wa kigeni, kutoka mataifa matatu tofauti kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno, aliwataja wachezaji wa kigeni aliowasajili kuwa ni Joseph Zziwa kutoka klabu ya Express FC ya Uganda, Ngamchiya Hamza (Cameroon) na kiungo mshambuliaji Sosthness Khakali (Kenya).

Alisema baada ya kumalizana na nyota hao, tayari wamekamilisha usajili wao kwa asilimia 90 na Kocha Mkuu mpya, Mmarekani Melis Medo, tayari ameanza majukumu yake kukinoa kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu mpya wa ligi hiyo.

"Kikosi tayari kimeingia kambini, tuko hapa hapa Tanzania na kocha wetu mpya, Medo ameanza majukumu yake ya kukinoa, matarajio yetu ni kufanya vizuri msimu huu kutokana na usajili tuliofanya kwa kuzingatia mapendekezo ya ripoti ya kocha aliyepita," alisema Mgweno.

Alisema wameboresha benchi la ufundi pamoja na kikosi cha timu hiyo kutokana na kutarajia ushindani mkubwa zaidi msimu huu huku wakitaka kufikia malengo yao na kuepuka kuponea mechi za mchujo (play off).

# HITIMANA, OMOG WATAJWA KUMRITHI BADRU MTIBWA

**Na Saada Akida**

KLABU ya Mtibwa Sugar bado inachanga karata zake vizuri, kutazama imwajiri kocha yupi kati ya Mrundi Thierry Hitimana ama Mcameroon Joseph Omog, baada ya kukiri kuwa katika mazungumzo na makocha hao waliowahi kuzinoa klabu mbalimbali hapa nchini kwa nyakati tofauti.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana ambaye aliwahi kuinoa Namungo pamoja na Mtibwa Sugar, alikiri kufanya mawasilino na uongozi wa klabu hiyo ya Manungu mkoani Morogoro kujadili uwezekano wa kurejea nchini kukinoa kikosi hicho kuelekea msimu ujao wa 2021/22.**

Alisema hawezi kusema lolote kuhusu mipango yake kwa sababu bado hawajafikia muafaka na klabu hiyo, ambayo aliachana nayo wakati Ligi Kuu msimu uliomalizika ikielekea mwishoni, kutokana na kutoelewana na msaidizi wake, Vincent Barnabas ambaye hayuko kwenye timu kwa sasa.

"Viongozi [wa Mtibwa] walinitafuta, wakanieleza mipango yao, mimi pia nimeweka mapendekezo yangu, bado mazungumzo hayajakamilika, hivyo wamenitaka nisubiri. Kwa upande wangu niko tayari kurejea kukinoa kikosi cha timu hiyo kama tukikubaliana," alisema Hitimana.

Hata hivyo, taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jijini jana kutoka ndani ya Mtibwa Sugar, tayari jina la Omog na Hitimana yameanza kujadiliwa na huenda mmojawapo akarejea nchini kukinoa kikosi cha 'Wakatamiwa' hao wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

"Kuna uwezekano mkubwa makocha hao, mmoja wao atarejea nchini maana Omog na Hitimana wote wanazungumza nao kati ya hao yeyote anaweza kuchukuwa nafasi ya Kocha Mohammed Badru ambaye naye anaandaliwa mkataba wa kupewa majukumu mengine ndani ya timu hiyo," kilieleza chanzo chetu ndani ya timu hiyo.

Kilisema ana imani kubwa ya kurejea kwa Hitimana baada ya viongozi kumpa nafasi kubwa kwa sababu bado huduma yake inahitajika, pia alikuwapo mwanzoni mwa msimu ulioisha lakini akaondoka kwa sababu ya kutokuwa na maelewano mazuri na Barnabas.

Alisema mambo yakiwa vizuri mmoja kati ya makocha hao atakuja kuchukua nafasi ya Badru aliyefanikisha timu hiyo kusalia katika ligi hiyo.

Kwa upande wa Omog, yeye aliwahi kuinoa Azam FC na Simba kwa mafanikio makubwa kabla ya kurejea kwao.

**TUMEMNASA...**



Mtendaji Mkuu wa Klabu ya DTB, Muhibu Kanu (Kushoto), akimtambulisha mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Mrundi Amissi Tambwe, tayari kuitumikia kwa msimu ujao wa Ligi Daraja la Kwanza. **PICHA: DTB**

## *Geita Gold hatarini kuikosa Ligi Kuu*

**Na Tunu Hassan,** TUDARCo

LICHA ya kupanda Ligi Kuu msimu huu, timu ya Geita Gold FC ipo kwenye hatihati ya kupoteza nafasi ya kushiriki ligi hiyo, kuelekea msimu huu wa 2021/22 baada ya kushindwa kulipa fedha inazodaiwa na waliokuwa wamiliki wa klabu hiyo wakati ikiitwa Mshikamano.

Geita Gold FC ilinunuliwa na wamiliki wa mgodi wa Geita wakati ikiitwa Mshikamano FC, jambo ambalo inaelezwa kwamba bado wanadaiwa takribani Sh. milioni 75 na waliokuwa wamiliki, Mshikamano FC.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kupitia Bodi yake ya Ligi (TPLB), klabu zote za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza, zinatakiwa kuwa Leseni za Klabu (Club Licensing), na moja ya vigezo katika leseni hiyo ni klabu kutokuwa na madeni.

Akizungumza na gazeti hili jana, aliyekuwa Mwenyekiti wa klabu ya Mshikamano, Victor Kowero, amesema bado hawajamalizana na Geita na ni mwaka wa nne sasa hakuna kilichofanyika na shauri lao limeshafika mpaka TFF.

Kowero alisema wanawashangaa Geita kwa nini hawataki kuwalipa mpaka sasa na hata kupunguza deni hilo wameshindwa kwa kipindi chote hicho.

Aidha, gazeti hili lilipomtafuta Mwenyekiti wa Geita Gold, George Mbiligenda, ili kuzungumzia madai hayo, alisema: "Naomba nisilizungumze kwa sasa kwa sababu suala hili linafuata michakato ya taratibu za kimaamuzi ya mahakama ya soka, ila ni suala ambalo lipo kwenye kamati. Hivyo naomba nisilitolee maneno yoyote, kwa sababu lipo kwenye mikono sahihi."

Michezo
Jumatano Agosti 25, 2021
Nipashe



Messi kuanza PSG, ikiivaa Reims UKURASA 22

# Manara sasa rasmi ni kijani na njano

Aahidi kuifanya kuwa matawi ya juu, awataka mashabiki kuacha kulalamikia...

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa Idara wa Habari na Mawasiliano wa zamani wa klabu ya Simba, Haji Manara, ameamua kuwa kijani na njano baada ya jana kutambulishwa kufanya kazi na klabu ya Yanga.

**Haji ambaye aliachana na Simba mwishoni mwa mwezi Julai baada ya kutokea kutokuelewana baina yake na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo, alitambulishwa jana saa 1:00 usiku kwenye Hoteli ya Serena, Dar es Salaam.**

Aliyetangaza tukio hilo lililoshangaza wengi ni Mshauri wa Masuala ya mabadiliko ndani ya klabu hiyo, Senzo Mazingisa.

"Haji karibu nyumbani, ukiona unanyayasika, rudi kwenu," alisema Ofisa Mhamasishaji wa klabu hiyo, Antonio Nugaz."

Akizungumza baada ya kutambulishwa, Manara alisema ataifanya kazi hiyo kwenye klabu ya Yanga mara kumi zaidi kuliko alivyokuwa akiifanya akiwa Simba.

"Rasmi nitangaze kuwa nimejiunga na klabu kubwa kupita zote Afrika Mashariki na Kati. Wapo watakaokwazika, wapo watakaochukia, lakini hii ni kazi kama kazi zingine zozote. Ni kama Kocha au mchezaji, makocha wanahama na wachezaji pia, hivyo na mimi naifanya hii kama kazi zingine.

"Nilipata ofa nyingi kutoka klabu mbalimbali, baadaye wakaja Yanga, kwanza nilishangaa, lakini nikaona wako 'siriasi', sikukataa," alisema Haji.

Haji ambaye alikuwa msemaji kwenye klabu ya Simba kwa miaka sita, na mtoto wa mchezaji wa zamani wa klabu ya Yanga, Sunday Manara, alipewa jezi na Senzo, akaivaa na kubusu nembo ya klabu hiyo.

"Jinsi nilivyokuwa naifanya kazi kule nilikotoka, huku nitaifanya mara 10 yake, tena nimekuja kwenye klabu ambayo imetwaa ubingwa mara 27 na nina uhakika kuwa msimu ujao vikombe vyote tutachukua na tutachukua ubingwa mara ya 28. Ila tu nawaomba, Yanga ni klabu kubwa haipaswi kuwa inalalamika, mara waamuzi mara nini, hapana tucheze mpira tushinde tuchukue makombe," alisema.

Kabla ya Manara kutambulishwa, Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa aliwataka wanachama na mashabiki wote kujitokeza kwa wingi Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika kilele cha Wiki ya Wananchi, akisema kuwa itakuwa ni tamasha la kutwa nzima, hivyo kuwahi mapema.

"Kutakuwa na mechi kadhaa za soka, wanamuziki na wasanii kutoka ndani na nje ya nchi, tutawatambulisha wachezaji wetu wote, mechi yetu dhidi ya Zanaco ya Zambia na 'sapraizi' nyingine kubwa ambayo itakuwapo," alisema.

Mfikirwa alisema klabu hiyo itazindua jezi zao leo hii kwenye Ukumbi wa Mlimani City ambapo baada ya hapo zitaanza kuuzwa kwenye maduka mbalimbali nchi nzima.

RASMI WETU...



Aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Haji Manara, akizungumza na waandishi wa habari baada ya Mshauri wa Masuala ya Mabadiliko ndani ya klabu hiyo, Senzo Mazingisa (kushoto), kumtambulisha rasmi kuwa mfanyakazi wa Klabu ya Yanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: YANGA**

## Ndemla, Ame ndiyo hivyo tena

**Na Tunu Hassan,** TUDARCo

WAKATI mashabiki wa Simba wakisubiri kuona ni wachezaji gani wanaachwa katika kikosi chao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa, tayari baadhi wametajwa kuanza kutafuta malisho kwingineko.

Kiungo mwenye mashuti makali ya mbali, Said Ndemla, ni mmoja wa wachezaji wa kikosi hicho cha Simba ambaye anahusishwa na kuondoka na kwenda kujiunga na KMC FC huku beki wa kati Ibrahim Ame akitajwa kuzungumza na Mtibwa Sugar.

Wachezaji hao wote walisafiri na timu kwenda kambini nchini Morocco, lakini wamerejea Dar es Salaam wakati wenzao wakiendela na mazoezi, hata hivyo, Kaimu Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ezekiel Kamwaga, alipoulizwa na mwandishi wetu kulikoni Ndemla na Ame wamerejea nchini wakati si miongoni mwa wachezaji wanaounda kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, alisema wameomba udhuru na wana jambo lao binafsi.

"Ndemla ana ruhusa rasmi kutoka kwa uongozi wa Simba ndiyo maana aliondoka kambini, zaidi ya hapo hakuna kitu kingine ambacho kimefika mezani kwangu. Hali kadhalika Ame naye aliomba ruhusu, kila mmoja ana jambo lake," alisema

Gazeti hili lilipomtafuta Katibu Mkuu wa Klabu ya KMC, Walter Harson, kuhusu klabu hiyo kuwa katika mazungumzo ya kumsajili Ndemla, alisema "Naomba nipe muda nitakueleza kitu cha uhakika kwa sababu nilikuwa msibani na jioni hii (jana jioni) tutasafiri na timu kwenda kuweka kambi Morogoro, nikifika huko nitazungumza na makocha na viongozi wenzangu kisha nitakueleza," alisema.

Kwa upande wa Ame, ambaye anahusishwa na Mtibwa Sugar, Msemaji wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, alipoulizwa alisema: "Tupo kwenye mazungumzo na nyota kadhaa kuelekea msimu ujao, kwa sasa siwezi kutaja ila hadi mwisho wa juma tutahitimisha zoezi zima na kuwatangaza nyota wetu. Tanzania ni nchi kubwa na ina timu nyingi na hatufanyi mazungumzo na wa ndani tu hata wa kigeni pia, tupo kwenye mawindo tusubiri mwishoni mwa juma hili."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >